BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,019,301,493/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

**MAKINDA** aeleza namna itakavyokuwa siku ya sensa





UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Agosti 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581027
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Wadau wapaza sauti kupanda bei mafuta

UKURASA 2






Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa vitabu vya mwongozo wa mafunzo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza na Balozi wa Korea ya Kusini hapa nchini, Sun Pyo Kim (katikati), baada ya kuuzindua katika Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana. Wengine ni Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said (kushoto), Mkurugenzi Mkazi wa KOICA Tanzania, Kyucheol Eo (wa pili kushoto) na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa. **PICHA: IKULU**

## Mwinyi aanika sababu za matokeo mabaya mitihani

UKURASA 2

UKURASA WA 3

### SERIKALI YATANGAZA NEEMA SEKTA YA NISHATI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amewataka Watanzania kutumia Kongamano la Kimataifa la Nishati 2022 kuongeza ujuzi na kujifunza namna ya kutumia fursa za ubia...

## Waziri Ummy aziwashia moto MOI na NHIF rushwa, utendaji

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, YANGA DIMBANI OKTOBA 23 UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia aliyekaa), akisikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WFM**

# Wadau wapaza sauti bei mafuta

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ikitangaza bei za mafuta kupanda zaidi kulinganisha na mwezi uliopita, wadau wamepaza sauti huku wakipendekeza mambo kadhaa ili kupunguza makali kwa wananchi.

Miongoni mwa mapendekezo hayo, wameomba serikali kupitia upya tozo na kodi za mafuta.

Juzi, EWURA ilitangaza bei mpya zitakazotumika Agosti huku kwa Dar es Salaam bei ya petroli ikipanda kwa Sh. 190 kwa kila lita, dizeli Sh. 179 na mafuta ya taa Sh. 323 kulinganisha na ilivyokuwa Julai.

Kwa mujibu wa taarifa ya EWURA, bei ya rejareja mkoani humo kwa mafuta ya petroli kwa sasa inauzwa Sh. 3,410 kutoka Sh. 3,220, dizeli Sh. 3,322 kutoka Sh. 3,143 na mafuta ya taa Sh. 3,765 kutoka Sh. 3,442 kwa lita.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Uchumi, Dk. Wilhelm Ngasamiaku, ameshauri kuwa njia pekee ya kupunguza makali kwa wananchi ni kuzipunguza tozo na kodi kwenye mafuta.

"Kuna tozo na kodi nyingi bado. Taasisi lukuki zina tozo zake kwenye mafuta. Njia pekee kuishusha hii bei ni kuzipunguza hizo tozo kwenye mafuta na taasisi nyingi ni za serikali ambazo zinachukua tozo kwenye mafuta.

"Hakuna namna nyingine zaidi ya hiyo mpaka mafuta kwenye soko la dunia itakapotulia na kushuka ambayo si leo. Zilifanyiwa mapitio lakini bado ni nyingi na kuna ambazo zinatakiwa kufutwa kabisa na zingine zipunguzwe ili kupunguza haya makali la sivyo tutaendelea kupata bei za juu za mafuta," alisema.

Kuhusu ruzuku ya Sh. bilioni 100 zinazotolewa na serikali, alisema kama isingeweka bei ya mafuta ingekuwa zaidi ya hiyo, mambo yangekuwa mabaya zaidi.

**LATRA YAFUNGUKA**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, alisema ni kweli bei zinapanda lakini wanapopanga tozo zozote, huzingatia utulivu wa soko la muda mrefu kwa maana kwamba isiwe bei ya kuyumba.

Alisema bei ya tozo za usafirishaji zilizowekwa zinahudumia mabadiliko hayo kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan kuna mchango wa ruzuku aliouingiza.

"Hii bei ingepanda zaidi ya hapo lakini fedha za Rais zimepunguza kasi ya kupanda kwa bei ya mafuta. Tunachojaribu kuangalia isifike mahali tukasema tupunguze bei kwa sababu vitu mara nyingi huwa vinapanda.

"Mpaka sasa hatujapata malalamiko na hatujaona kama kuna haja ya kufanya mapitio ya bei za usafirishaji kwa sababu bado zilizopo hazijafikia bei kikomo iliyowekwa, lakini sheria haizuii kama tukiletewa malalamiko ya kufanya mapitio.

"Mapitio yanaweza kufanyika wakati wowote kutokana na hali inavyoweza kutokea, ukijaribu kutizama bado kuna watu (vyombo vya usafiri) wanapiga debe kuita abiria kwa bei ya chini ikilinganishwa na iliyopo kwenye soko, ukishaona hivyo kumbe huyu mtu anaweza kuliendesha gari lake kwa bei ya chini au likiwa na abiria wachache," alisema.

Suluo alisema LATRA inatambua bei ya mafuta inavyopanda kwa sababu huathiri gharama nyingi za bidhaa hivyo wamekuwa wakifanya ufuatiliaji kwa kushirikiana na wadau.

**TAMKO TABOA**

Mkurugenzi wa Habari wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustapher Mwalongo, alisema wanatarajia leo kutoa maoni yao kuhusu kupanda kwa bei za mafuta, baada ya kikao walichokiitisha.

**BEI KWA SASA**

Kwa mujibu wa taarifa ya EWURA , bei mpya zilizotangazwa zinajumuisha ruzuku ya Sh. bilioni 100 iliyotolewa na Serikali ambapo isingekuwapo lita ya petroli ingekuwa Sh.3,630 na dizeli Sh.3,734 kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ilisema bei ya mafuta katika soko la dunia zimeendelea kuongezeka na kusababisha katika soko la ndani nazo kupanda.

Kwa Mkoa wa Tanga bei ya petroli bila ruzuku ni Sh. 3,584 na baada ya ruzuku ni Sh 3,435 wakati Mtwara kabla ya ruzuku ni Sh. 3,762 na baada ya kuiweka imekuwa Sh. 3,393.

Taarifa hiyo imetaja bei za dizeli kwa Mkoa wa Tanga kabla ya ruzuku 3,929 na baada ya kuiweka imekuwa Sh. 3,349 na Mtwara kabla ya ruzuku ni Sh. 3,933 na baada ya kuiweka imekuwa Sh. 3,351.

**MADEREVA**

Dereva wa daladala inayofanya safari kati ya Segerea na Kawe, Muhidini Fundisha, alisema wanatarajia kupeleka mapendekezo yao kwenye mamlaka husika ili ifikirie namna ya kuongeza nauli zitakazoendana na kupanda kwa mafuta.

Naye Rama Hussein, dereva wa bodaboda, aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kuweka bei ya mafuta ambayo itasaidia kupunguza makali kwao kuliko zinavyopanda kila mwezi.

Mwendesha bodaboda jijini Mwanza, Hamis Maghembe, alisema bei za mafuta zinawaathiri kibiashara kwa sababu nauli zipo pale pale.

Mwendesha bajaji jijini Arusha, Dickson Martin, alisema ongezeko la bei ya mafuta itasababisha wao kuongeza nauli pamoja na bei ya vyakula kupanda maradufu.

Kwa upande wake, mkazi wa Mwanza, Bruno Damas alisema nauli zinavyozidi kupanda zinasababisha bidhaa kupanda na kuiomba serikali kuviangalia upya viwango vya bei ya mafuta ili wananchi wasiendelee kuumia.

Mkazi wa Babati, mkoani Manyara, Ramadhani Mohamed, alisema ni vizuri serikali iangalie eneo la kuongeza tozo kwa kuzipunguza ili kufidia mafuta yasiendelee kupanda.

■ **Imeandaliwa na Romana Mallya na Maulid Mmbaga (Dar) Peter Mkwavila na Magdalena Jackson (Dodoma), Richard Makore (Mwanza), Allan Isack (Arusha), Angela Mhando (Siha), Jaliwason Jasson (Manyara) na Hamida Kamchalla (Tanga).**

# Dk. Mwinyi aanika sababu matokeo mabaya mitihani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2017 hadi 2021, matokeo ya mitihani ya Taifa ya kumaliza elimu ya sekondari hayakuwa mazuri huku akiweka bayana sababu zilizofanya kuwapo kwa hali hiyo.

Amesema uhaba wa walimu, maabara na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa vitendo hasa kwa masomo ya hisabati na sayansi ndivyo vilisababisha ufaulu huo kuwa duni.

Kutokana na sababu hizo, amesema wastani wa asilimia 33 ya wanafunzi kila mwaka hukosa vyeti vya kumaliza masomo na wengi wao ni wale wanaosoma masomo ya sayansi.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa mafunzo ya walimu wa sayansi, hisabati na Kiingereza pamoja na makabidhiano ya miongozo ya mafunzo, uliofanyika katika hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Alisema kutokana na matokeo hayo, serikali iliamua kutafuta mbinu za kunusuru hali hiyo na kuwezesha kiwango cha elimu na ufaulu kupanda.

Katika kutimiza azma hiyo, alisema serikali itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo ikiwamo kuwajengea walimu uwezo zaidi wa ufundishaji, kujenga maabara za sayansi na kuzipatia vifaa.

"Nafurahi kusikia kwamba tulianza kuwapatia mafunzo walimu 600 wanaofundisha kidato cha kwanza na cha pili kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza kupitia Mradi wa ZISP ambao serikali inautekeleza kwa ushirikiano na Benki ya Dunia.

"Leo (jana) tena kwa kushirikiana na KOICA, tutawapatia mafunzo walimu wa shule za sekondari wa kidato cha tatu na cha nne wanaofundisha masomo hayo Unguja na Pemba," alisema Dk. Mwinyi.

Pia alisema mradi wa kuimarisha elimu ya sekondari wa kuwajengea uwezo wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza walimu unakwenda sambamba na mikakati ya serikali ya kuhakikisha inatoa elimu bora inayoendana na mahitaji ya sasa.

Dk. Mwinyi alisema elimu kwa masomo ya sayansi na hisabati ina mchango mkubwa katika kufikia malengo hayo, hivyo ni lazima mikakati imara ya kuinua ufaulu wa masomo hayo na uwezo katika lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi uimarishwe.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Leila Mohammed Mussa, alisema kabla ya msaada wa KOICA wa kutoa mafunzo kwa walimu wa sayansi wa sekondari, pia imesaidia ujenzi wa maabara 10 za kisasa ya sayansi Unguja na Pemba.

Alizitaja juhudi za serikali katika kuimarisha elimu ikiwamo kutenga Sh. bilioni 63 kwa ajili ya miradi ya elimu ambazo zinatokana na fedha za ahueni ya UVIKO-19.

Balozi wa Korea ya Kusini nchini, Sun Pyo Kim, alisema serikali ya nchi yake itaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika miradi yake ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu.

Mkurugenzi Mkazi wa KOICA, Kyucheol Eo, alisema kuna hatua mbalimbali ambazo Korea Kusini inachukua katika kuiunga mkono Zanzibar kwenye sekta ya elimu huku akiahidi kuendeleza misaada zaidi ili kuhakikisha masomo ya sayansi, Hisabati na Kiingereza yanafundishwa kwa ufanisi mkubwa.

# Serikali yatangaza neema sekta nishati

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amewataka Watanzania kutumia Kongamano la Kimataifa la Nishati 2022 kuongeza ujuzi na kujifunza namna ya kutumia fursa za ubia na kampuni za kimataifa katika sekta ya gesi na mafuta nchini.

Vilevile, ameahidi serikali itaendelea kusimamia kikamilifu sekta ya nishati nchini ili kuondoa kero mbalimbali zitokanazo na sekta hiyo.

Jijini Dar es Salaam jana, Majaliwa alitoa kauli hiyo alipolifungua kongamano hilo la siku mbili, lililohudhuriwa na mamia ya washiriki kutoka nchi 25 waliowakilisha kampuni zinazoshughulika na sekta hiyo.

Waziri Mkuu Majaliwa, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alisema: "Umeme tulionao utaimarika na utakuwa wa gharama nafuu, na sasa tuna uhakika wa kupeleka umeme mpaka vijijini na tunaendelea kuhamasisha Watanzania kila mmoja aweke umeme."

Alisema kuwa mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda unaendelea vizuri, akisisitiza kuwa kampuni inayosimamia utekelezaji wa mradi huo imejipanga vizuri kwa pande zote mbili za Tanzania na Uganda.

Majaliwa alisema utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya nishati, ikiwamo mafuta na gesi, utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi wa nchi kutokana na mapato yatakayokuwa yanakusanywa kutoka kwenye miradi hiyo.

Alisema kongamano hilo litafungua fursa za uwekezaji nchini kutokana na kujumuisha kampuni kubwa za kimataifa katika sekta ya nishati.

"Tuna wageni ambao ni wadau katika sekta ya nishati, kongamano hili la kimataifa litafungua fursa zilizopo kwenye sekta ya nishati ikiwamo maji, makaa ya mawe, gesi na umeme wa jua," alisema.

Majaliwa alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na washirika wa kimataifa katika kukuza ushirikishwaji na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika sekta ya nishati.

"Lengo la serikali ni kutumia fursa za sekta yetu ya nishati ili kuboresha sekta nyingine ikiwamo viwanda na uchumi. Hivyo, ni kwa imani yangu kwamba kongamano hili litawawezesha washiriki kubadilishana uzoefu, mawazo, ujuzi na maarifa ambayo ni muhimu katika kusimamia rasilimali za mafuta kwa njia endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho," alihimiza.

Pia, alisema serikali itaendelea kuhakikisha inaweka kanuni na taratibu zinazofaa ili kuwezesha ushirikishwaji wa wafanyabiashara wa ndani kunufaika na mnyororo wa thamani katika sekta ya nishati.

"Ujio wa kampuni hizi ni fursa katika kuchochea majadiliano na uhusiano wa uwekezaji kwenye sekta hii, kutoa uelewa mpana wa fursa na kujadili kero na namna ya kukabiliana nazo ili kuimarisha uchumi wa nishati," alifafanua.

Majaliwa alisema Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 imeweka wazi mazingira ya kuchochea ushiriki wa kampuni za wazawa huku Sera ya Nishati inahimiza kuishirikisha sekta binafsi kwa lengo la kuimarisha uchumi unaogusa maisha ya Watanzania.

Alisema serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya kuwezesha kampuni za wazawa ili kuhakikisha zinanufaika na mnyororo wa fursa zilizopo katika sekta hiyo ya gesi na mafuta.

"Kwa sasa majadiliano ya Mkataba Hodhi (HGA) ili kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) yanaendelea na yatafungua ukurasa mpya katika uchumi wa taifa letu.

"Mwezi Desemba tutatia saini mkataba wa mwisho kisha uzalishaji utaanza kwa kuzingatia maelekezo nya kiongozi wetu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan," Majaliwa alisema na kusisitiza kuwa mazungumzo ya mradi huo mkubwa yanakwenda vizuri chini ya usimamizi wa Wizara ya Nishati.

Kampuni na taasisi mbalimbali za Kitanzania, yakiwamo mashirika ya umma yanayohusika na sekta hiyo, yameandaa mabanda kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere linakofanyika kongamano hilo kwa ajili ya kutoa elimu na kuendesha majadiliano kwa washiriki.

Waziri wa Nishati, January Makamba, katika hotuba yake kwenye kongamano hilo jana, alitangaza fursa za uwekezaji na utalii zilizopo nchini, akitamba kuwa Tanzania kwa miongo mingi imekuwa nchi yenye amani na usalama.

Alisema kongamano hilo ni fursa muhimu kwa kupata uelewa na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya nishati, hasa mafuta na gesi nchini.

Waziri January alisema kongamano la mwaka huu linatarajiwa kuwakutanisha washiriki zaidi ya 800, akidokeza kwamba waliokuwa wamejisajili hadi jana walikuwa zaidi ya 1,000.

Alisema watalitumia kongamano hilo kueleza hali ya miradi yao ikiwamo Bwala la Julius Nyerere, ukachakati wa gesi asilia na mingine mingi.

Aliwapongeza waandaaji wa kongamano hilo, Ocean Business Partners, akisisitiza kuwa litakuwa na manufaa makubwa, hasa kwa sekta ndogo ya gesi na mafuta nchini na ulimwenguni kwa ujumla.

Awali, Mkurugenzi wa Ocean Business Partners ambao ndiyo waandaaji wa kongamano hilo, Abdulsamad Abdulrahim, alisema kongamano hilo litawawezesha wadau kutambua fursa za uwekezaji katika sekta ya nishati nchini.

# Ummy aziwashia moto MOI, NHIF

Na Martha Magawa



WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameziwashia moto Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhusu tuhuma za rushwa na zuio la matibabu kwa zaidi ya hospitali moja ndani ya siku 30.

Ummy alisema hayo jana wakati akizungumza na Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) baada ya kuizindua jana jijini Dar es Salaam huku akiwataka watumishi wa taasisi hiyo na bodi kutoa huduma zinazoridhisha kwa wagonjwa na kujiepusha na rushwa.

"Nawaomba JKCI mzidishe huduma bora kwa wagonjwa. Madaktari simamieni maadili ya kazi yenu, epukeni masuala ya kuomba na kupokea rushwa. Nimepokea kesi za MOI kadhaa, madaktari wakituhumiwa kuomba rushwa ili kuhudumia wagonjwa," alisema Ummy.

Pia aliwaagiza JKCI kuanzisha vituo vya kudumu katika hospitali za kikanda ikiwamo Hospitali ya Chato ambayo itakuwa kituo cha matibabu ya moyo kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mikoa mingine inayotakiwa kuanzishwa matibabu ya moyo ni Mtwara na Mbeya huku Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ikitakiwa kuanzisha huduma za kibingwa za mifupa.

**NHIF 'STOP'**

Waziri Ummy pia alipiga marufuku utaratibu mpya wa NHIF ambao unazuia mgonjwa kutibiwa katika zaidi ya hospitali moja kwa muda wa siku 30.

Katika zuio hilo, NHIF iliangaza kuwa kuanzia mwezi huu, mgonjwa anatakiwa atibiwe kituo kimoja ndani ya siku 30.

Alisema utaratibu huo ulikuwa na nia njema lakini NHIF haikuzingatia masuala muhimu ikiwamo kukaa na wadau wao katika huduma ili kuja na mbinu mbadala ya kudhibiti udanganyifu ambao unasababisha hasara kwa mfuko huo.

"NHIF wana wazo zuri la kudhibiti na kupunguza hasara inayosababishwa na ongezeko la gharama za matibabu lakini hawajafuata utaratibu sahihi ikiwamo kupokea maoni ya wadau," alisema.

Pia aliiagiza NHIF kutotumia utaratibu huo bila kufikishwa Wizara ya Afya ili upitiwe kabla ya kutumika kwa wananchi huku akiwataka wananchi kuacha mara moja tabia ya kuhama hospitali ndani ya muda mfupi kwa kuwa tabia hiyo husababisha usugu wa maradhi.

NHIF ilitoa utaratibu kuanzia Agosti Mosi, mwaka huu, hospitali zinazotoa huduma kupitia mfuko huo kutopokea mgonjwa ambaye ametibiwa hospitali nyingine kabla ya siku 30 kumalizika isipokuwa awe amepata rufani kwenda kutibiwa kituo kipya au ikiwa ni dharura na lazima maelezo ya dharura hiyo yawe ya kujitosheleza.

Mfuko huo ulisema lengo lilikuwa kupunguza wagonjwa kuhama vituo, huku wagonjwa waliokutana na kadhia hiyo kadi zao zilikuwa zikishindwa kusoma.

**NEEMA MATIBABU MOYO**

Katika hatua nyingine, Ummy alisema serikali kupitia wizara yake iko kwenye mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango ili wagonjwa wa moyo wanaotibiwa ndani, walipiwe gharama za matibabu kama wale wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi.

Alisema kupitia JKCI serikali imeokoa fedha zilizokuwa zikipeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi na kwamba iko haja kuwafikiria wanaopatiwa matibabu katika taasisi hiyo ambao wanashindwa kumudu gharama za matibabu.

"Mgonjwa akipelekwa nje kwa matibabu serikali inalipia. Kwa nini wagonjwa wa ndani wasipate pia fursa hiyo? Wizara tuko kwenye mazungumzo na Hazina na muda si mrefu tutakuja na mwafaka wa hili," alisema.

Pia aliwataka kutositisha huduma kwa mgonjwa anayeshindwa kulipia matibabu badala yake wafanye tathmini ya mgonjwa huyo ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza kipindi wanapositisha huduma.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema taasisi hiyo imeokoa Sh. bilioni 51 toka ilipoanzishwa kiasi ambacho serikali ilikuwa ikitumia kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi.

Janabi pia alisema taasisi hiyo imeshafanya upasuaji mkubwa wa kifua 2,769 pamoja na mdogo 8,065 toka ilipoanzishwa na asilimia 85 ya madaktari wanaofanya upasuaji huo ni Watanzania.


Victoria Finance

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ADIMILO REUBEN MSUYA | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO – KONGOWE | JOFORTE AUCTION MART | 18-08-2022 |
| 2 | CHARLES NTYUKI MHOJA | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO - MOROGORO | HOLLYNESS & RESPISHERS COMPANY LIMITED | 18-08-2022 |
| 3 | VUMILIA ALLY MPUTA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - MOROGORO | HOLLYNESS & RESPISHERS COMPANY LIMITED | 18-08-2022 |
| 4 | ESTHER MOSSES FIKIRINI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- TABATA KINYEREZI | JOFORTE AUCTION MART | 18-08-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

116976701

# Makinda aeleza itakavyokuwa siku ya sensa

**Na Waandishi Wetu**

KAMISAA wa Sensa, Anne Makinda, amebainisha namna watu watakavyohesabiwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Pamoja na kubainisha hayo, amesema kwamba sensa hiyo itafanyika kwa siku sita huku akifafanua kuwa hakutakuwa na mapumziko wakati huo.

Akizungumza jana sensa hiyo itakavyokuwa, Makinda alisema kazi hiyo itafanyika kuanzia Agosti 23 saa 6:01 usiku na kwamba itaendelea hadi muda wa siku sita. Alisema watakaokuwa safarini watapewa vitambulisho maalum ili wasihesabiwe mara mbili.

"Kuna makarani ambao wamepangiwa katika maeneo maalumu hususani wanaosafiri usiku kuanzia saa 6:01 usiku wa kuamkia siku ya sensa, tayari watakuwa katika maeneo hayo na watawauliza maswali machache tu na kisha kuwapatia vitambulisho, ili huko wanakokwenda wasihesabiwe tena," alisema Makinda.

"Kazi hii haiwezi kuisha kwa siku moja, tumeweka muda hadi siku sita, ili kuhakikisha kazi hii inafanyika kwa ufasaha.

"Kila karani atakuwa na kiongozi katika eneo lake alilopangiwa, ambaye ni msimamizi wa maudhui, kwa hiyo atapanga ratiba aanzie mitaa ipi kwa siku hiyo ya kuamkia siku yenyewe ya sensa hadi kumaliza katika muda ambao umepangwa," alisema.

Makinda alisema taarifa za msingi karani anatakiwa kupata anapofika ni idadi ya watu walioamkia Agosti 23 kwenye kila kaya.

"Kwa hiyo hata ikiwezekana ni vema siku ya sensa kila kiongozi wa kaya akaandika idadi ya watu wake walioamkia siku hiyo ya sensa kwenye kaya yake, ili kuepusha kusahau kwa sababu huenda karani asimfikie siku hiyo," alisema Makinda.

Maeneo mengine ambayo alisema ni maalum ambayo wataanza kuhesabu makarani kuanzia saa 6:01 ni hospitalini, viwanja vya ndege na bandarini.

Pia alisema kwa kundi la watoto wa mitaani nako kuna makarani ambao wamepangwa kwa ajili ya kazi hiyo.

"Yaani sensa hii itapita kwenye maeneo yote, hakuna litakaloachwa, hata vijiweni huko nako watafikiwa. Na katika yale maeneo ambayo ni hatarishi tumepanga makarani wa kiume," alibainisha.

Kuhusu maeneo ya jeshi, Makinda alisema huko watafanya wenyewe na watapewa mafunzo kama inavyofanyika kwa makarani wengine.

"Kwenye maeneo ya jeshi raia hawaingii, watafanya wenyewe huko isipokuwa watapewa mafunzo kama makarani wengine kwa ajili ya kazi hizo, kwa hiyo hata kwa wafungwa gerezani watafanya wenyewe huko,"alisema Makinda.

Alisema makarani waliopewa mafunzo kwa ajili ya kazi hiyo watakula kiapo cha kutunza siri na kwamba endapo atakuwapo atakayevunja kiapo hicho na kutoa siri atachukulia hatua ikiwamo kifungo cha miaka miwili au faini.

Makinda ambaye ni Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania, alisema baadhi ya maswali yatakayoulizwa siku ya sensa kwa kaya ni pamoja na idadi ya wanakaya, elimu yao, kama kuna wenye ulemavu na ni wa aina gani na shughuli wanazofanya

"Na huenda karani akataka kuona kitambulisho chochote ulichonacho iwe ni cha udereva, uraia, cheti cha kuzaliwa au kama una namba ya NIDA.

"Na katika hapa nataka wananchi waelewe kuwa si kwamba hawatohesabiwa wasipokuwa na hivyo vitambulisho, lengo ni kutaka kujua idadi ya wananchi wenye vitambulisho vya taifa ili tunapoishauri serikali tuseme ni asilimia ngapi wana vitambulisho.

"Na katika hili naomba pia ikiwezekana waviandae kabisa, ili karani akifika wanamwonyesha tu na si kwenda kutafuta maana inaweza kupoteza muda," alisisitiza.

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR) na Loyce Cyriacus (SJMC)**




Mwananchi akipita kwenye mbao iliyowekwa kwa ajili ya kuvukia kukwepa matope katika eneo la barabara ya soko la Kigogo Fresh Pugu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wamwomba Chongolo kurudishiwa soko

**Na Mary Geofrey**

WAFANYABIASHARA wa soko la samaki Manyema, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamemwomba Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kurudishwa sokoni hapo baada ya halmashauri kuwaondoa Machi mosi, mwaka huu.

Wafanyabiashara hao walimpigia magoti Katibu Mkuu Chongolo jana katika eneo la Mawenzi, baada ya kuwasili kwa ajili ya kuweka jiwe la msingi mradi wa nyumba za wafanyabiashara akiwa kwenye ziara yake wilayani Moshi.

Wakizungumza kwa sauti ya kulia, walimwomba Katibu Mkuu huyo wa CCM kuielekeza halmashauri iwarudishe eneo hilo kwa sababu soko walilopelekwa la Bomambuzi Kata ya Pasua, hakuna wanunuzi.

"Tunaomba, tunaomba baba tunateseka, tunateseka baba, huu sio umri wa kuteseka," alisikika Fatma Yusuph, mkazi wa Njoro, mmoja wa wafanyabiashara hao.

Wanawake hao wakiwa wamepiga magoti na majani mikononi, walisema tangu waondolewa kwenye soko hilo wanashindwa kufanya biashara na kupata kipato cha kuendesha familia zao.

Chongolo alilazimika kumwagiza Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, kutoa ufafanuzi kuhusu suala hilo.

Kayanda akitoa ufafanuzi alisema, halmashauri ilitumia mapato ya ndani kutenga fedha kwa ajili ya kujenga na kukarabati soko la Pasua ili litumike kwa ajili ya biashara ya samaki.

"Sehemu wanayoisema ambayo walikuwa wakifanyia biashara ilikuwa ya chini ambayo hata kiafya haikuwa salama.

"Lakini kupitia kikao cha baraza la madiwani na vikao mbalimbali liliidhinisha fedha," alisema huku akikatishwa na kelele za wananchi waliokuwa wakizomea.

Chongolo alilazimika kuingilia kati akisema: "Sikilizeni, waungwana hawapigi kelele, muungwana hafanyi hivyo, subirini kwanza amalize. Subirini kwanza, mheshimiwa DC endelea."

Mkuu wa wilaya, aliendelea kusema halmashauri ilitenga Sh. milioni 250 kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye soko la Pasua na kujenga vyoo maeneo mengine ili wafanyabiashara wapate huduma katika mazingira salama na mazuri kiafya.

Aidha, alisema eneo la awali miundombinu ilikuwa sio salama kwao kufanya biashara.

Chongolo alimkatisha kwa kumhoji kama soko la samaki la Manyema likikarabatiwa litafaa kuendelea kutumika na wafanyabiashara hao.

"Je, soko hili linaweza kutengenezeka likaanza kutumiwa na wafanyabiashara kuuza samaki zao?"

Akijibu swali hilo, Kayanda alisema, "eneo hilo linafaa kuendelea kufanya biashara endapo litafanyiwa ukarabati."

Alipoulizwa kama kuna tathmini yoyote imefanyika kujua kiasi kinachohitajika kufanya ukarabati, alidai kuwa hawajawahi kufanya tathmini yoyote kuhusu ukarabati huo.

Chongolo alitoa siku saba kwa halmashauri kufanya tathmini ya bajeti inayohitajika.

Alisema wakifanya kupata gharama halisi za kiwango kinachohitajika wasukume upatikanaji wa fedha na kufanya ukarabati.

"Naomba nimwachie DC, atumie wataalamu kujua fedha zinazohitajika aniletee ndani ya wiki moja tukishajua gharama mimi nitasaidia kusukuma zipatikane ili lifanyiwe ukarabati," alisema Chongolo.

Tangazo la kuwaondoa wafanyabiashara hao lilitoka Februari 17, kuwa Machi Mosi, 2021 walitakiwa kuondoka kwenye soko hilo na kuhamia soko la Bomambuzi.

Chongolo yupo mkoani Kilimanjaro kwa ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhimiza sensa ya watu na makazi.

## Mama aliyetelekeza watoto watatu ajisalimisha polisi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MWANAMKE aliyetelekeza watoto watatu wa kike kisha kwenda kuolewa katika kijiji kingine, Adelyda Nakashawa, amejisalimisha polisi baada ya kusakwa na vyombo vya dola kwa muda mrefu.

Nakashawa ambaye ni mmoja wa wazazi wawili (wanandoa) waliotelekeza watoto wao watatu wa kike katika Kijiji cha Gombe wilayani Ulanga na kusababisha kukosa ulinzi na malezi ya baba na mama.

Mzazi huyo wa kike, amelazimika kujisalimisha polisi baada ya amri ya Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, kutaka yeye na mume wake, Thomas Ulanda, wasakwe popote walipo ili kuwajibishwa kutokana na mabinti hao kutelekezwa kwenye nyumba chakavu, bila chakula wala malazi na malezi na kwenda kuolewa na kuoa vijiji vingine walikokuwa wakiishi.

Malenya aliyeingilia kati tukio la kutelekezwa kwa mabinti hao wanafunzi, alikiri kujisalimisha kwa mwanamke huyo, ambaye katika mahojiano amemtupia lawama mzazi mwenzie wa kiume kuwa ndiye aliyefanya utelekezaji huo baada ya yeye kumwachia watoto na kwenda kuolewa kwingine.

Licha ya mwanamke huyo kujisalimisha, mkuu huyo wa wilaya ameagiza kuendelea kusakwa kwa baba mzazi wa watoto hao ambaye amedaiwa kuhama kutoka eneo moja hadi lingine kutokana na kusakwa na polisi.

"Nimeagiza vyombo vya sheria vifanye jukumu lake. Hadi sasa serikali ya kijiji cha Gombe imetoa eneo la ekari moja kwa ajili ya kuwajengea mabinti hawa makazi na kupata hati ya majina yao.

"Pia John De Vries, Mwenyekiti wa Black Rock Mining na kampuni ya uchimbaji madini ya Graphite maarufu kama Kinywe ya Faru Graphite Corporation, ameridhia kuwajengea watoto hao nyumba itakayogharimu zaidi ya Sh. milioni kumi na kujali mahitaji yao yote ya msingi yakiwemo elimu na malazi," alisema.

Pia amesema serikali ya wilaya inaendelea kuratibu mradi wa Msichana Wetu (Our Girl) uliofanikisha kuwaibua mabinti hao ili kupunguza changamoto za mtoto wa kike wilayani Ulanga.

"Agosti 4 (leo) pia kutakuwa na kikao cha bodi ya mradi wa Our Girl ambayo mimi kama mwenyekiti nitapokea taarifa ya kaya maskini zenye mtoto wa kike na kuendelea kuzitatulia ufumbuzi. Naendelea kuwaasa wazazi kutimiza majukumu ya kulea kwani hakuna mtoto wa mtaani. Hawa watoto wana wazazi wao," aliongeza.

Binti mkubwa anayetegemewa na wenzake wenye umri wa miaka 13 na tisa, Elionida Ukanda (17), ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Selina Kombani, awali alisema mama yao aliwaacha wakati akiwa darasa la sita mwaka 2017 na kuwaacha na baba yao.

Alisema mama yao huyo aliondoka tena Novemba, mwaka huo huo, kisha baba yao naye akaondoka na kuwaacha peke yao.

# Ofisa polisi aeleza alivyojifanya mfanyabiashara meno ya tembo

**Na Grace Gurisha**

OFISA wa Polisi aliyekuwa katika Kituo cha Polisi Mburahati, Dar es Salaam, Inspekta Festus Simon, ameieleza Mahakama jinsi alivyoweka mtego wa kumkamata mfanyabiashara wa meno ya tembo kwa kujifanya anataka kununua jino moja kwa Sh. 150,000. Inspekta Simon amedai kuwa aliweka mtego huo baada ya msiri wake kumpa namba ya simu ya mshtakiwa, Hassan Abdallah, huku akimrubuni kuwa anafanya biashara ya meno ya tembo.

Simon alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Evodia Kyaruzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakati akitoa ushahidi dhidi ya Abdallah. Inspekta Simon alidai kuwa, kwa sasa yupo Kituo cha Polisi Bunda mkoani Mara anapofanyia kazi.

Alidai Januari 3, 2019 akiwa ofisini kwake, alipata taarifa kutoka kwa msiri kuwa kuna mtu anafanya biashara ya meno ya tembo na anatafuta mnunuzi wa vipande vinane.

"Msiri alinipa namba ya simu ya Abdallah nikaanza kufanya naye mawasiliano nikijitambulisha kuwa mimi ni mfanyabiashara nataka kununua meno ya tembo," alidai Inspekta Simon. Alidai kuwa katika mazungumzo hayo, walikubaliana Januari 4, 2019 wakutane eneo la Uwanja wa Sahara, ambapo alimweleza mkuu wake wa kazi kuhusiana na taarifa hizo.

Baada ya kumpa taarifa hizo, alidai kuwa mkuu wake wa kazi alimpa askari mwingine wa kumsaidia kukamilisha mpango wa kumkamata mshtakiwa huyo.

Shahidi huyo alidai kuwa kabla hawajakutana na mtuhumiwa, alimpa masharti kwamba asiende na mtu mwingine katika biashara hiyo kwa sababu watu si waaminifu wasije wakakamatwa.

"Nilimwambia sawa lakini nitaenda na mwenzangu ninayefanya naye biashara hiyo, kwa hiyo tutakuwa wawili. Abdallah alikubali mimi kwenda na mtu mwingine," alidai Inspekta Simon.

Alidai kuwa siku ya tukio alikwenda eneo la Uwanja wa Sahara akiwa na askari mwenzake wakiwa wamevaa kiraia na kumpigia simu mshtakiwa kwamba wameshafika eneo la biashara na walikubaliana kununua meno hayo kwa Sh. 150,000 kwa kila jino. Inspekta Simon alidai wakati wanamsubiri waliona taksi yenye ufito wa Illa ambapo mtuhumiwa alishuka ndani ya gari akiwa amebeba begi jeusi na kwenda sehemu ambayo wao walikuwapo.

"Alituuliza kama tunamzani, tulimwambia upo kwenye buti la gari, akafungua begi na kutoa jino moja akisema mzigo ni mzuri huku akitoa jino lingine. Askari mwenzangu alimshika mkono na kumweka chini ya ulinzi na kumfunga pingu," alidai.

Shahidi huyo alidai wakati wanaendelea kumdhibiti mtuhumiwa, dereva wa teksi aliyempeleka aliondoka eneo hilo na kutokomea.

Inspekta Simon alidai wakiwa eneo hilo la tukio walijaza fomu ya ukamataji mali na kutiwa saini na mshtakiwa pamoja na shahidi huru, Shabani Hamis, na baadaye mtuhumiwa alifikishwa kituo cha polisi.

Hakimu Kyaruzi aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 17, mwaka huu, kwa kuendelea kusikilizwa.

# Mtaalamu afichua wanandoa kupata tatizo afya ya akili

**Na Magdalena Jackson,** SJMC

MTAALAMU wa Saikolojia ya Afya ya Akili wa Hospitali ya Mirembe, Roselyne Malenya, ametaja baadhi ya sababu za wanandoa kupata tatizo la afya ya akili ikiwamo mabadiliko ya majukumu.

Malenya alisema vitendo vya mauaji na kujeruhiwa kwa wanandoa ni moja ya dalili za tatizo la afya ya akili.

"Hali hii hujidhihirisha kutokana na vichocheo mbalimbali katika ndoa kama vile kutokutambua majukumu yao katika familia kutokana na mabadiliko ya kimajukumu," alisema.

Alisema kuwa majukumu yaliyokuwa yakitimizwa na wanaume kipindi cha nyuma, sasa yanatimizwa na wanawake na kusababisha kutojua mahali pakusimama kama wanandoa kwenye majukumu yao.

Kwa upande wake, Dk. Sulma Islam, mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), alisema sababu ya malezi kwa watoto ni tatizo kubwa kwa vijana linalochangia kupata tatizo la afya ya akili.

"Hii inatokana na kukosa ukaribu wa wazazi hivyo kushindwa kupata watu wa karibu wa kuwaeleza changamoto wanazopitia mtaani, shuleni hata nyumbani," alisema.

Dk. Islam alisema tatizo la afya ya akili pia linatokana na kurithi kwa ugonjwa huo na mtu mwenye vinasaba hivyo dalili zake hujitokeza kwenye masomo au kazini.

"Hawa wakurithi dalili za ugonjwa wa afya ya akili hujidhihirisha kupitia matendo mbalimbali kama vile mauaji, ubakaji na kuchoma nyumba," alisema.

Aidha, Daktari Bingwa wa Afya ya Akili katika hospitali hiyo, Dk. Sadik Mandari, alisema wagonjwa wengi wanaowapokea hospitalini wenye tatizo la afya ya akili ni waliofanya uhalifu mtaani na kuhifadhiwa kitengo cha Isanga.

"Wagonjwa hawa huletwa kufanyiwa uchunguzi kama wametenda uhalifu huo kwa kukusudia au ni kwa sababu ya ugonjwa wa akili na ikigundilika kuwa wamefanya hivyo kutokana na afya ya akili wanatakiwa kukaa hospitalini kwa miaka mitatu kwa ajili ya matibabu mpaka atakapokuwa tayari kurudi nyumbani," alisema.

Mkurugenzi wa Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paulo Lawala, alibainisha walivyojipanga kusaidia jamii yenye tatizo hilo huku wakizindua gari litakalosaidia kutoa tiba ya afya ya akili maeneo ya vijijini.

"Uzinduzi huu wa huduma za afya ya akili kwa jamii, pia ni sehemu ya huduma zingine za kijamii, tunategemea kuwa na mbio za kuhamasisha afya ya akili kwenye jamii na mdahalo wa kitaifa wa afya ya akili utakaofanyika mwezi Septemba, mwaka huu," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema, utafiti uliofanyika mwezi Julai, mwaka huu, Tanzania ina wagonjwa wa afya ya akili kati ya 6,000 - 7,000 na kutokana na idadi hiyo taasisi ina hakikisha inaongeza elimu kwa jamii kupunguza tatizo hilo.

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **HERA-TRUST COMPANY LIMITED, JOSINA COMPANY LIMITED, J & J RECOVERIES, LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD na BROVITAS COMPANY LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | HERA-TRUST COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | ROSALINA ROGATUS KAMAFA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | YANGEYANGE-MSONGOLA-DAR ES SALAAM |
| 2 | DAUDI M CHACHA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NO.560, KITALU L | MBAGALA ZAKHEM-DAR ES SALAAM |
| 3 | SALOME AMIRIUS MWAILENGE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | TABATA CHANGOMBE-MFAUME STREET- DAR ES SALAAM |
| 4 | LAURENCE A LEKULE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | PUGU-BOMBANI-DAR ES SALAAM |
| 5 | PAUL PETER MALILO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KINYEREZI- DAR ES SALAAM |
| | J & J RECOVERIES | | |
| 6 | FROLIAN CHOGO SIMONI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KICHANGANI-KINYEREZI-DAR ES SALAAM |
| 7 | THERESIA ALEXANDER KITARY | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MSIGANI-UBUNGO-DAR ES SALAAM |
| 8 | JUBILET LUSINDE MACKDORNARD | SHAMBA LENYE MKATABA WA MAUZIANO- MALI YA VERONICA BENARD MALUGU | TENGELEA-MKURANGA-PWANI |
| 9 | APOLINARY PETER MWAMBONA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO-MALI YA PETER ISAYA LESIRWA | NZASA A-KILUNGULE-TEMKE-DAR ES SALAAM |
| 10 | DAVID JOSIA OBAS | PAGALE LENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIVULE-ILALA-DAR ES SALAAM |
| | BROVITAS COMPANY LIMITED | | |
| 11 | IDDI I IDDI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BOMBAMBILI-SONGEA |
| 12 | FROLA B KOMBA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO-MALI YA AMANI F MTAULEHE | NAMTUMBO-SONGEA |
| 13 | EMMANUEL N MAPUNDA | VIWANJA VYENYE HATI MILIKI KIWANJA NO.133 NA 135, KITALU A | MSHANGANO-MTENDEWAWA-SONGEA |
| 14 | JACOB NICODEM YAYA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KIWANJA NO.1417, KKITALU QQ | MJIMWEMA-SONGEA |
| 15 | FRANCIS ANDREA NDUNGURU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NAMANYINGI-SONGEA |
| 16 | EMMANUEL SOSTENES MSABILA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KIWANJA NO. 68, KITALU RR | RUVUMA-SONGEA |
| | LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD | | |
| 17 | OSCAR S MNG'ONGO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NO 210, KITALU P | CHAUNGINGI-NJOMBE |
| 18 | RIZIKI S MGAYA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI-INAYOMILIKIWA MERLY CHAULA NA KIWANJA CHENYE HATI MILIKI NO.54, BLOCK A | MGENDELA NA NJOSS A-NJOMBE |
| 19 | GASTON D MBAVILE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO NA GARI AINA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI T438 BAL | MJIMWEMA-MSETE-NJOMBE |
| 20 | PLASDO D MAULAGA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KIWANJA NO.915 | KAHAWA-MAKAMBO |
| 21 | MORBERT G NYOMOLELO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | IGANGIDUNGI-MAKAMBAKO |
| 22 | LEAH A NDELWA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | NUNDU-IBOMA-NJOMBE |
| | JOSINA AUCTION MART LTD | | |
| 23 | FREDY MALI KAZI | PAGALE LENYE HATI MILIKI KIWANJA NO 614, KITALU A | MHONGOLO-KAHAMA |
| 24 | DANIEL N MAGITA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI NO.576, KITALU A | BUSOKA-KAHAMA |
| 25 | EMMANUEL S MASHIGNI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KAGONGWA-KAHAMA |
| 26 | MUSSA ALLY TENELA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI KIWANJA NO.45, KITALU J | NYIHOGO-KAHAMA |
| 27 | BENJAMIN M BIKINDU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NGUZO MBILI-GEITA |
| 28 | KAGENGELE J MANDATA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYANTORONTORO A -GEITA |
| 29 | EDSON RASHID METHSULA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | LUTOZO-CCM-GEITA |
| 30 | SAMWEL J MAGODI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | SENGEREMA |
| 31 | MAULID A MTWALE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | 14 KAMBARAGE-GEITA |
| 32 | HUSSEIN H SELEMAN | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BUSERESERE-KATORO-GEITA |
| 33 | EMMANUEL JOHN KADISA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MWIME-KAHAMA |

### MASHARTI YA MNADA

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano ya benki na mnunuzi.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

### KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Hera-Trust Company Limited S.L.P Dar es Salaam**
**Namba za simu:**
**0654 673880**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji.**
**J & J Recoveries**
**S.L.P Dar es Salaam**
**Namba za simu;**
**0714292260/0784 076588**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**JOSINA COMPANY LIMITED**
**S.L.P MWANZA**
**Namba za simu:**
**0713203040/0789203040**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**BROVITAS COMPANY LIMITED S.L.P Songea**
**Namba za simu;**
**0763801591**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD**
**S.LP Dar es Salaam**
**Namba za simu; 0682272906**

**NA**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu:**
**0768790399, 0754774949**

216975901

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mpango wagonjwa wa moyo kulipiwa matibabu habari njema

**WAGONJWA** wa moyo wanaweza kupata matumaini ya kulipiwa gharama za matibabu baada ya jana Waziri wa Afya, kutangaza kuwa serikali kupitia wizara yake iko kwenye mazungumzo na Wizara ya Fedha ili wagonjwa hao wanaotibiwa ndani walipiwe gharama kama wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi.

Tangazo hilo la waziri alilitoa wakati akizindua Bodi ya Wadhamini wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Kupitia Taasisi ya JKCI tumeelezwa kuwa serikali imeokoa fedha zilizokuwa zikipeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi na kuona haja ya kuwafikiria wanaopatiwa matibabu katika taasisi hiyo ambao wanashindwa kumudu gharama za matibabu.

Nia hiyo ya serikali inatoa matumaini makubwa hasa kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kulipa gharama kubwa na maisha hayo kuwa katika wasiwasi.

Matumaini yetu ni kuona mazungumzo hayo yanazaa matunda na kama alivyosema Waziri Ummy kama mgonjwa akipelekwa nje kwa matibabu serikali inalipia, kwanini wagonjwa wa ndani wasipate pia fursa hiyo.

Wananchi tunasubiri kwa hamu kubwa na tunaombea mazungumzo hayo yanafanikiwe ili kuokoa maisha ya wagonjwa wasiokuwa na uwezo.

Suala lingine ambalo hatuna budi kumpa kongole Waziri Ummy ni la kutambua umuhimu wa kumpa huduma mgonjwa anayeshindwa kulipia matibabu kwa kumfanyia tathmini ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza kipindi wanapositisha huduma.

Umuhimu pia uliotolewa kwa kinamama na watoto hasa kwa kaya duni ambazo zinashindwa kumudu gharama za matibabu pamoja na wazee kwa kutorudishwa nyumbani ni wa kupongeza na kama alivyosema waziri kwa kutofanya hivyo, tunapoteza rasilimali watu.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alieleza jinsi taasisi hiyo ilivyookoa mabilioni ya fedha toka ilipoanzishwa kiasi ambacho serikali ilikuwa ikitumia kupeleka wagonjwa wa moyo kutibiwa nje ya nchi.

Na kwamba taasisi hiyo imeshafanya upasuaji mkubwa wa kifua kwa wagonjwa 2,769 pamoja na mdogo kwa wagonjwa 8,065 toka ilipoanzishwa huku asilimia 85 ya madaktari wanaofanya upasuaji huo ni Watanzania.

Hatua hii ni ya kujivunia kuona madaktari wetu wana uwezo wa kufanya upasuaji huo ambao miaka ya nyuma ilikuwa lazima ufanyike nje ya nchi.

Pia, inajenga imani kubwa kwa Watanzania kuona madaktari wazawa wana utaalamu huo ambao ulikuwa ukifanywa na madaktari wa nje.

Mwenyekiti wa Bodi, Prof. William Mahalu, anawahakikishia Watanzania kuwa jukumu kubwa la taasisi hiyo ni kuondoa au kupunguza asilimia tano ya wagonjwa ambao bado wanalazimika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu ya moyo.


Kadhalika ni kuhakikisha JKCI itaendelea na utaratibu wake wa kutoa mafunzo kwa mabingwa nchini ili kuongeza huduma za kibingwa ndani na kupunguza gharama kwa serikali.

Watanzania wanamatumaini makubwa na hospitali zao kutokana na kuwa na madaktari wenye uwezo mkubwa ambao pia wanaaminiwa na nchi za nje.

Tunasubiri kwa hamu mazungumzo yatakavyokuja na habari njema ya kuwaokoa wagonjwa wa moyo wasiokuwa na uwezo ili nao waweze kufaidika na fedha za serikali yao.

**Mungu ibariki Tanzania**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wiki ya Unyonyeshaji ikumbushe ulazima, umuhimu wa kunyonyesha

Na Jenifer Gilla

**MWEZI** Agosti unapoanza unakuja na ujumbe mahususi kwa jamii, wanawake, wanaume na vijana wanakumbushwa umuhimu wa maziwa ya mama kwa mtoto.

Kuanzia Agosti mosi hadi saba kila mwaka dunia inakuja pamoja kuadhimisha Siku ya Unyonyweshaji Maziwa ya Mama iliyoidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ili kuhamasisha unyonyeshaji watoto wadogo na wachanga.

Akifungua maadhimisho hayo kwa mwaka huu wilayani Ikungi mkoa wa Singida, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Mwanaidi Khamisi, anasema unyonyeshaji wa watoto wachanga ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa umeongezeka hadi kufikia asilimia 90 ukilinganishwa na asilimia 54 ya mwaka 2018.

Hata hivyo, anaongeza kuwa ni asilimia 43 pekee ya watoto hunyonyeshwa kwa miaka miwili na kuendelea huku asilimia 57 wakinyonya maziwa ya mama pekee bila kuchanganya na chakula kingine kwa miezi sita.

Pongezi ziende kwa wanawake wote walioitikia wito na mafunzo ya madaktari na kunyonyesha watoto wao maziwa ya mwanzo ambayo kitaalamu huitwa 'colostrums' ambayo yamejaa virutubisho, madini ya kutosha tena ya aina mbalimbali na protini kwa wingi.

Yana rangi ya njano yamejaa seli za kinga za aina mbalimbali na huwalinda watoto dhidi ya magonjwa ya binadamu na vifo.

Utafiti wa kitabibu unaeleza kuwa mtoto akizaliwa na kuanzia kunyonyeshwa maziwa ya mama ndani ya saa moja kuna uwezekano wa kuokoa maisha yake kwani kuchelewa kumnyonyesha mtoto kunachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya watoto wachanga ndani ya siku 28.

Aidha, changamoto bado inaonekana kwenye unyonyeshaji wa watoto kwa kipindi cha miaka miwili na kuendelea kwa kuwa wazazi wengi huishia mwaka hadi mwaka na nusu kwa sababu mbalimbali.

Moja ya sababu inayotawala kwa wazazi wengi ni kuwa wakinyonyesha kwa miaka miwili maziwa yao yanalegea na kupoteza mvuto na mwonekano jambo ambalo si sahihi na ni ukatili kwa watoto hao.

Tunafahamu kuwa kunyonyesha maziwa ya mama kuna faida nyingi kwa mama na mtoto ikiwamo kunaimarisha afya, kinga na ustawi wa mama na mtoto.

Aidha, ni mwanzo wa kuzuia aina zote za utapiamlo kwa kuwa mtoto anapata lishe bora iliyosheheni kwenye maziwa ya mama.

Ikumbukwe kuwa vile vile, mtoto asiponyonyeshwa ipasavyo huathiri ukuaji na maendeleo yake kimwili na kiakili kwa kuwa hatapata lishe bora inayomkinga dhidi ya magonjwa na kusababisha vifo vya watoto nchini.

Ili kufanikisha hilo, wazazi hawana budi kuhakikisha kuwa wanajiepusha na mambo yanayoweza kuathiri afya ya watoto wao kiakili na kimwili.

Kadhalika, mama asiponyonyesha anajisababishia msongo wa mawazo kwa kuwa utafiti unaonyesha kuwa utengenezaji maziwa ya mama mwilini, pia unahusisha saikolojia ya mama mwenyewe.

Hii ina maana kuwa kama una mawazo mengi, msongo wa mawazo au umechoka basi utoaji wa maziwa utapunguza na ndiyo maana kinamama wengi wanakuwa hawatoi maziwa ya kutosha.

Hivyo basi, kama Naibu Waziri Mwanahamisi alivyoisihi jamii kuadhimisha Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama , Watanzania wakumbuke umuhimu wa kuboresha lishe kwa watoto kwa kuanza kuwanyonyesha mara mama anapojifungua.

Unyonyesha sahihi unakataza kuwalisha watoto kitu chochote ndani ya miezi sita . Ikumbukwe unyonyeshaji wa maziwa ya mama ili kujenga msingi imara wa afya na uhai wa watoto ambao ni taifa la kesho ni muhimu kwa kila mzazi..

Kwa kuwa Ripoti ya WHO inaonyesha kuwa kati ya watoto watano, watatu hawanyonyeshwi ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, maisha ya watoto zaidi ya 820,000 ya chini ya miaka mitano yangeweza kuokolewa ikiwa watoto wote wa miezi 0 mpaka 3 watanyonyeshwa kikamilifu.

Wazazi na jamii isipuuze tuwainue kiafya watoto wetu kwa kuwanyonyesha kikamilifu.

# RC mpya aanza na ajenda ya mapato

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU mpya wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, ametua mkoani hapo na kuagiza halmashauri zote kumpa mikakati yao ya ukusanyaji wa mapato ili kuusogeza mbele mkoa.

Malima alifika katika ofisi zake jijini Mwanza jana asubuhi na kupokewa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Robert Gabriel, na viongozi wengine huku akiwataka watendaji kuweka wazi mikakati yao katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema ukusanyaji wa mapato ni ajenda yake ya kwanza katika mkoa huo wenye idadi ya watu wanaofikia milioni nane kwa sasa.

Malima alisema, watu milioni sita wanaishi Mwanza na kwamba wengine milioni mbili ni wale wanaoingia na kutoka kila siku hivyo ni lazima wingi huo wa watu uendane na ukusanyaji wa mapato.

Aliongeza kuwa, mkoa huo una idadi kubwa ya watu na kwamba ni lazima uendane na upatikanaji wa mapato mengi kuliko mikoa mingi hapa nchini.

"Ndugu zangu ajenda yangu ya kwanza ni kuhakikisha Mwanza inasonga mbele kimapato kwa kuwa ni miongoni mwa mikoa ya kimkakati na hili nitalifanya kuwa ajenda yangu ya kwanza," alisema Malima.

Alisema anaufahamu vizuri mkoa huo na kwamba Rais Samia Suluhu Hassan amemwagiza ahakikishe unasonga mbele kuliko ulivyo sasa.

Malima ambaye amewahi kufanya kazi katika mikoa ya Mara na Tanga, aliwataka watendaji kushirikiana ili kumsaidia Rais na kwamba ni lazima ajenda ya wananchi katika kujiletea maendeleo ifanikiwe.

Akizungumza baada ya kumkabidhi ofisi, Gabriel alisema anaondoka ofisini akiwa hana 'nongwa' na mtu yeyote.

Alisema katika uongozi wake alishirikiana na viongozi wenzake wa mkoa na kwamba maendeleo ya wananchi na ulinzi na usalama alivifanya kwa nguvu zote.

Gabriel aliongeza kuwa miradi mingi ilianzishwa katika kipindi chake na kwamba mpaka anaondoka kulikuwa na mradi wa ujenzi wa vyumba 11,000 vya madarasa katika mkoa mzima.

Alimshukuru Rais Samia na kwamba kwa sasa anaondoka ofisini kwenda kufanya kazi za Chama Cha Mapinduzi (CCM), kama mjumbe wa shina nafasi ambayo alisema aliwahi kuitumikia huko nyuma.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akiwa amebebwa juu na washiriki wa mashindano ya Bodaboda (Tanzania Royal Tour Rally -2022), baada ya kuweka jiwe la msingi la uzinduzi wa ujenzi wa nyumba ya mshindi wa kwanza wa kitaifa wa mashindano hayo, Iyumbu jijini Dodoma. **PICHA: CCM**

# Shaka ataka vijana kushirikishwa mipango ya maendeleo kwa uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amewataka viongozi wa chama na serikali kuwashirikisha vijana katika mipango ya maendeleo.

Katika kufanya hivyo, amesema ni kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amewekeza nguvu kubwa kuliinua kundi hilo kiuchumi kupitia fursa mbalimbali zilizoko nchini.

Shaka aliyasema hayo juzi jijini hapo wakati akizindua ujenzi wa nyumba ya mshindi wa kwanza atakayepatikana katika mashindano ya mbio za waendesha bodaboda kitaifa, yanayotarajiwa kuhitimishwa Agosti 30, mwaka huu, yakiwa na lengo la kuunga mkono juhudi za Rais Samia katika kutangaza fursa za utalii nchini kupitia filamu ya The Royal Tour.

Alisema CCM inaamini vijana wakiwezeshwa kiuchumi wana uwezo wa kuchangia maendeleo ya taifa kwa kiwango kikubwa zaidi na ilivyokuwa sasa.

"Tanzania tunaye mwongoza njia, mfungua fursa ambaye ni Rais Samia mwenye kutekeleza dhana na maono ya kuwakomboa vijana kiuchumi kupitia fursa na rasilimali zilizoko nchini. Rais Samia amefanya uwekezaji mkubwa katika kuwainua vijana.

"Jitihada hizi zinapaswa kuendelea kuungwa mkono kwa viongozi wa chama na serikali kuwashirikisha vijana katika mipango ya maendeleo. Hii itasaidia kutekeleza kwa vitendo ahadi ya CCM ya kutoa ajira milioni nane kwa sekta rasmi na isiyo rasmi," alisema.

Shaka pia alisema CCM inaamini kwamba endapo vijana watawezeshwa zaidi kiuchumi, watachangia maendeleo ya taifa kwa hatua kubwa zaidi ya sasa.

Alibainisha kuwa mbio hizo za waendesha bodaboda ni fursa ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko pamoja na waendesha vyombo hivyo vya moto kuwa mabalozi wazuri wa utalii.

Shaka alitumia fursa hiyo kuwahamasisha waendesha bodaboda na bajaji kushiriki sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu, pamoja na kuendelea kupata chanjo ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Global Peace Advocacy for Conflict Resolution, Ryamoja Mfuru, alisema taasisi hiyo imeandaa mashindano hayo kuwawezesha waendesha bodaboda kubeba ujumbe wa kuhamasisha utalii nchini.

Alisema mbio hizo ngazi ya wilaya zitaanza Agosti 13, mwaka huu, kisha Agosti 17 zitaendelea kwa ngazi ya mkoa na kuhitimisha kitaifa Agosti 30 ambapo mshindi atakabidhiwa nyumba iliyoko jijini Dodoma. Naye Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, alisema CCM imekuwa na ushirikiano mzuri na Umoja wa Waendesha Pikipiki Mkoa wa Dodoma (UWAPIDO) na imetoa ofisi kwa ajili ya uendeshaji shughuli za chama hicho.

Mwakilishi kutoka kampuni ya State Aviation, Amour Abdallah, alisema kampuni hiyo itatoa helikopta kuhamasisha tukio hilo kwani uwezeshaji vijana husussan madereva bodaboda ni msaada muhimu katika kuchangia maendeleo ya taifa.

# UDSM yabuni jiko mionzi jua

**Na Martha Sambo,** MBEYA

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimebuni jiko la kupikia linalotumia mionzi ya jua, ili kupunguza uharibifu wa mazingira kwa ajili ya kuni na mkaa.

Akizungumza na Nipashe, mbunifu wa jiko hilo ambaye ni Mhandisi wa chuo hicho cha UDSM, Alphen Mlelele, alisema baada ya kufanya utafiti alibaini mwanga wa jua unaweza kutumika kupika chakula.

Alisema walibuni teknolojia hiyo ili kutunza mazingira kutokana na ukataji miti ovyo hali inayochangia mabadiliko ya tabianchi.

"Tuliona tubuni teknolojia hii ya kutumia nishati ya jua kupikia chakula ili kurahisisha, lakini kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambayo mara kadhaa yanahatarisha mazingira na utunzwaji wake kwa ujumla, hivyo tukaona ni wakati sahihi hakufanya hivyo," alisema Alphen.

Pia, alisema jiko hilo linapunguza gharama ya gesi na umeme hasa vijijini ambako matumizi ya mkaa na kuni yanatokana na baadhi ya watu kushindwa kumudu gharama ya bidhaa hiyo.

"Awali tulifanya utafiti tukagundua jiko hili linafaa kutumika kwenye mikoa yenye kipindi kirefu cha jua ikiwamo Njombe, Iringa, Mbeya, Dodoma na Singida," alibainisha Alphen.

Ripoti ya pili ya hali ya mazingira nchini ya mwaka 2014, ilibainisha kuwa zaidi ya hekta 46,942 za misitu huharibiwa kwa shughuli za mkaa na kilimo.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Iringa, Dk. Bahati Goliama, alisema mkoa huo umepoteza zaidi ya Sh. bilioni 281 katika kipindi cha 2021 kwa sababu ya uchomaji wa misiti ovyo.

Alisema kama misitu hiyo isingechomwa na miti yake kufikisha umri wa miaka 16, mkoa ungejipatia Sh. bilioni 491.

# Shule yawapunguzia kero umbali mrefu wanafunzi

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa** SIHA

WANAFUNZI wa Kijiji cha Naibii, Kata ya Biriri, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, wanatarajia kuondokana na adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 12 kwenda Shule za Sekondari Makiwaru na Sanya Juu, baada ya serikali kujenga Shule ya Sekondari Biriri.

Ujenzi wa shule hiyo mpya, ulihusisha madarasa manane, jengo moja la maktaba, matundu 28 ya vyoo, chumba cha teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), maabara sita za masomo ya sayansi na jengo la utawala, uko katika hatua za mwisho za kukamilika. Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Joel Mgalula, akisoma taarifa ya ujenzi huo juzi kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alisema umegharimu Sh. milioni 470.

"Mradi huu pia kutimiza azma ya serikali ya kuwa na shule za sekondari kwa kila kata ambayo pia ni maelekezo ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020, sura ya kwanza D (ii), 9E (ii) na sura ya tatu 79 (i)," alisema Mgalula.

Alisema majengo yote yamegharimu Sh. milioni 468.3 na utekelezaji wa mradi huo unakadiriwa kuwa umefika asilimia 85.

"Tumeahidiwa kupewa fedha Sh. milioni 130 katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 202/25," alisema.

Katibu Mkuu Chongolo, aliagiza ujenzi huo kukamilika mapema ili wanafunzi waanze masomo mapema mwakani.

Aidha, aliahidi kuzungumza na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ili shule hiyo iwe na masomo ya kilimo kwa ajili ya kuandaa vijana kujiajiri katika sekta hiyo.

Mwananchi wa kijiji hicho, George Mchome, alisema kuwapo kwa shule hiyo kutasaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi kwa sababu watakuwa na muda mrefu wa kujisomea wanaotumia sasa kwenda shule za mbali.

Chongolo yupo mkoani Kilimanjaro kwa ziara ya siku tano ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/25, miradi ya maendeleo na kuhamasisha Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha Benki ya NBC, Mussa Mwinyindaho, akizungumza kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo, kama mikopo ya mitaji, ujenzi wa jengo la biashara na Bima ya Biashara, wakati wa mkutano na wafanyabiashara wa mkoa wa Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NICOL yaendelea kufanya vizuri

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya NICOL Investment PLC, imeendelea kupata faida na hisa zake kuendelea kufanya vizuri katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa, faida ya kampuni hiyo imepanda kutoka Sh. bilioni 1.5 mwaka 2020 mpaka bilioni nne mwaka 2021.

Hisa za kampuni hiyo kwenye soko la hisa nazo zimeonekana kuendelea kupanda kwa kasi kutoka Sh. 200 mwaka 2020 hadi Sh. 360 mwaka huu.

Akizungumzia siri ya mafanikio hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NICOL, Erasto Ngamilaga, alisema ni kweli mapato ya kampuni hiyo ya kizalendo yanaendelea kupaa kwa kasi.

Alisema wakati kampuni hiyo inasajiliwa DSE mwaka 2018 ilikuwa na changamoto nyingi lakini kwa sasa mambo yako safi na wanahisa wanafurahia kampuni yao kuendelea kufanya vizuri huku wakilipwa magawio na kupata taarifa za kampuni kwa uwazi.

Ngamilaga alitaja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni kampuni kufanya mikutano ya kila mwaka na kwa mfululizo kuanzia mwaka 2018 wanahisa kuendelea kupata gawio la faida mfululizo.

Alisema hivi karibuni walitangaza hesabu zilizokaguliwa zinazoonyesha kuwa faida ya kampuni hiyo imekua kutoka Sh. bilioni 1.5 mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 4 mwaka 2021.

Kwa mujibu wa ofisa huyo mtendaji mkuu, hilo ni sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 144 na kwamba mafanikio hayo yamechangiwa na mapato wanayopata kutoka kwenye magawio na mapato yanayotokana na riba baada ya kufanya uwekezaji kwenye hati fungani.

"Mafanikio haya yamekuja kutokana na jitihada za makusudi tunazoendelea kuzifanya katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi sasa na kuendelea, hayo yamewezekana baada ya kuchukua juhudi za kutawanya uwekezaji wetu kwenye maeneo yenye faida kubwa hasa kwenye hati fungani," alisema.

Alisema wanaendelea na jitihada za kutawanya uwekezaji wa kampuni ili kuufanya uwiane na malengo ambayo kampuni imejiwekea kwa kuzingatia mkakati wa kukuza mapato na faida kwa manufaa ya wanahisa wake.

Hivi karibuni, alisema ulifanyika mkutano wa dharura wa wanahisa ili kuthibitisha uchaguzi wa wakurugenzi wapya na wanahisa walithibitisha na kuteua wakurugenzi wapya.

"Tumefanikiwa kujaza nafasi kwa mujibu wa maazimio ya wanahisa yaliyofikiwa katika mkutano mkuu wa saba, ni matumaini ya wanahisa kwamba wakurugenzi walioteuliwa wataongeza chachu ya maendeleo ya kampuni pamoja na kukidhi matakwa ya sheria katika uendeshaji bora wa kampuni unaoziingatia weledi," alisema.

Mtendaji huyo alisema yapo maeneo mengine makubwa ya kimkakati ambayo kampuni inaendelea kuwekeza mbali na kuhakikisha kwamba mapato yanayopatikana kwenye gawio na hati fungani yanarejeshwa katika uwekezaji mwingine.

Alisema NICOL inatathmini kuingia kwenye uwekezaji wa viwanda na maeneo mengine, tunaendelea kufanya tathmini ya kufanya uwekezaji katika maeneo mengine kama vile uwekezaji katika sekta ya gesi, milki, madini na uanzishwaji wa mifuko mbalimbali itakayoongeza tija.

Alisema mwaka 2021 wanahisa walithibitisha gawio la muda la Sh 17 ambalo lililipwa Desemba 30, mwaka jana, na kwamba wanahisa waendelee kuwa na matumaini makubwa.

"Ni matarajio yetu kwamba kulingana na mafanikio makubwa tuliyo nayo wanahisa waendelee kutarajia mazuri kwenye mkutano wa wanahisa unaokuja tutakaoufanya, tarehe ya mkutano huo itatangazwa," alisema.

# Mfumuko wa bei, pembejeo kujadiliwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imeonyesha nia ya kumaliza kilio cha wakulima nchini, kuhusu mfumuko wa bei ya pembejeo za kilimo kwa ahadi ya kutangaza Agosti 8, mwaka huu, wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane).

Kaimu Mrajis wa Vyama Vya Ushirika nchini, Collins Nyakunga, akizungumza wakati wa warsha ya uwekezaji ya wanahisa wa KCBL, kuelekea uundwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika, alisema serikali itatangaza ahueni ya kushuka kwa bei ya mbolea, baada ya kuweka ruzuku kupunguza makali.

Nanyunga ambaye alimwakilisha Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, alisema ni wakati wadau wa ushirika taasisi binafsi, Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro na serikali zikiangalia namna bora ya kuongeza mtaji wa KCBL, kufikia Sh. bilioni 15, na kwamba hivi sasa serikali inapitia mapendekezo na changamoto zinazowakabili wakulima na itatangaza hatima yake mwezi ujao.

Awali, Meneja wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro, Godfrey Ng'urah, akieleza mafanikio, mkakati na muundo kuelekea uundwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika, alisema Vyama vya Akiba vya Kuweka na Kukopa (SACCOS), vinatarajiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 10.2, wawekezaji wa kimkakati, itakusanya Sh. bilioni 4, Vyama vya Ushirika wa Wakulima (AMCOS), itakusanya zaidi ya Sh. 3.8 ili kufikia malengo ya Sh. bilioni 15 zinazohitajika.

Katika mkutano huo wa uwekezaji, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Dk. Emmanuel Lulandala, akieleza nafasi ya Benki ya Ushirika katika ushindani wa soko huria na sekta binafsi, amesema sehemu ya mfumo wa uchumi inayoendeshwa na watu binafsi au makampuni ili kutengeneza faida na haidhibitiwi na serikali.

Kwa mujibu wa Dk. Lulandala, Benki ya Ushirika (BU) ni fursa ya wana ushirika kumiliki uchumi na kutengeneza faida kubwa, ambayo ni mali ya wanachama wa vyama na vyama ambao ndio wamiliki na kwamba ushirika lazima ushindane kumiliki uchumi.

Kulingana na takwimu za Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) za mwaka 2021, Tanzania ina jumla ya vyama vya ushirika 9,741 wakati idadi ya wana ushirika nchini imefikia watu milioni 6,900,000 na nguvu ya fedha ya wana ushirika ni Sh. bilioni 717.5.

## Makada 36 CCM wajitokeza kuwania ubunge A. Mashariki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKADA 36 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi ya ubunge wa Afrika Mashariki huku wengine wakitetea ubunge wao.

Akizungumza juzi jijini hapo, Katibu Msaidizi Mkuu Idara ya Oganaizesheni CCM, Solomoni Itunda, alisema wanachama hao wamechukua fomu ofisi ya makao makuu ya CCM Dodoma, ofisi kuu ya CCM Zanzibar na ofisi ndogo ya CCM, Dar es Salaam.

Alisema kwa juzi na jana makada 36 wamejitokeza kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa kuwania ubunge huo.

Alitaja wanachama waliochukua fomu kuwa ni Amani Kajuna, Azizi Mussa, Judith Mollel, Amedeus Mzee, Kalunde Malale na William Reuben, Fancy Nkuhi, Salma Mwassa, Ngwaru Maghembe, Happyness Lugiko, Shabu Makonyola, Salimu Kungulilo, Prof. Norman Sigalla, Harrison Lukosi, Rehema Hassan, Ahmed Mkulo, Steven Mkomwa, Dorica Gwilenza na Ansar Kachabwa.

Wengine ni Nadra Juma Mohamed, Ahmed Shehe Saleh, Mar-yam Said Mussa na Mourie Oscar Sendera, Jonas Lufungulo, Dk. Linda Salekwa, Loti Lembrice, Richard Mbuguni, Angela Kiza, Pascal Mayala, Francis Nanai, Melinda Muganda, Fikiri Luganga, Mkondo Fabian, Albert Mbago, Robison Etuttu na David Mwakanjuki.

Alitoa wito kwa wanachama wengine wenye vigezo kujitokeza kuwania nafasi hizo ili kutimiza takwa la kikatiba.

CCM ilitangaza uchukuaji wa fomu kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo kuanzia Agosti mosi - 10, mwaka huu.

# Wizara yaweka mkakati wanaofanya ukatili kijinsia kunyimwa dhamana

**Na Martha Magawa**

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu imesema imejipanga kuweka mkakati kwa wanaofanya ukatili wa watoto na wanawake wasipate dhamana ili kuzuia kufanya matukio mengine wakiwa uraiani.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mwanaid Khamis, kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida wakati akipokea taarifa ya wilaya hiyo iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya, Jerry Muro.

Mwanaid alisema kuwa mkakati huo utajikita na kuweka sheria ya kutokuwapatia dhamana kwa mtu yeyote atakayefanya ukatili wowote kwa wanawake na watoto nchini, ili wanaofanya matukio hayo wasipate dhamana na kuepusha matukio mengine watakapokuwa uraiani.

"Inasikitisha sana na ukatili unaoendelea hivi sasa nchini, nina imani hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote wanaofanya matukio ya kikatili ikiwamo ya kutoa uhai," alisema Mwanaid.

Awali, akitoa taarifa kwa Naibu Waziri, Mkuu wa wilaya alisema, wilaya yake imejikita kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa kushirkiana na mabalozi wa SMAUJATA hussan kipindi cha mavuno ambacho kinakuwa na matukio ya mauaji ya wanawake katika maeneo ya vijijini.

Alisema ukatili wa watoto na wanawake bado unaendelea na wilaya bado inaendelea kutoa mkazo kwa kuwatafuta wahalifu na kuwakamata ili sheria zichukue mkondo wake.

"Tunapambana nao wale wote wanaofanya ukatili kwa watoto na wanawake tunahakikisha tunawakamata, tangu matukio haya yanayotokea kwenye wilaya yetu, tumewakamata wale wote wanaofanya ukatili huu na tunazidi kutoa elimu na Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii."

Muro alibainisha kuwa hivi karibuni wanawake wawili kutoka vijiji tofauti katika Wilaya ya Ikungi, waliuawa kikatili na wanaume zao.

Kwa mujibu wa ripoti ya Jeshi la Polisi iliyotolewa mwaka 2021, kuna ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili dhidi ya watoto huku mwaka 2020 visa 7,388 viliripotiwa kote nchini tofauti na mwaka 2015, matukio 5,803 yaliripotiwa.



Mkulima wa matikiti katika Kijiji cha Malongwe mkoani Tabora, Esther Lema (kulia), akihudumia moja ya mashamba yake kijijini hapo, juzi. Kilimo hicho, kimemnufaisha na kumwezesha kulima ekari mbili kwa sasa kutoka nusu kwa mwaka jana. Kushoto ni Msaidizi wake, Nicolaus Mwakasiju. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Elimu ujasiriamali yawainua wanufaika TASAF

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

UTOAJI wa elimu ya ujasiriamali kwa wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani Mbogwe mkoani Geita, imewafanya wanufaika kuelekeza fedha wanazozipata katika shughuli za uzalishaji mali ikiwamo kilimo na ufugaji wenye tija na kuwakwamua kiuchumi.

Wanufaika hao walisema hayo wakati walipotembelewa na maofisa wa TASAF kwa lengo la kuangalia shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanufaika husasani katika sekta za kilimo, afya, elimu na maji.

Mmoja wa wanufaika hao, Gaitaba Mashinzi mkazi wa kijiji cha Shibutwe alisema, alianza kupokea Sh. 58,000 fedha ambazo alizielekeza kwenye shughuli ya kilimo cha zao la mpunga na alipopata fedha baada ya mavuno alinunua mbuzi na mpaka sasa anao saba na kuku 17.

Alisema, kutokana na elimu ya ujasiriamali wanayoipata mara kwa mara hususani nyakati za kupatiwa fedha imewafanya kuachana na matumizi mabaya ya fedha ikiwamo unywaji wa pombe na kuzielekeza katika shughuli za kimaendeleo.

Mashinzi alisema, kabla ya uwapo wa TASAF alikuwa akiishi maisha magumu ya kutegemea vibarua vya kulima mashamba ya watu na alishindwa kutimiza mahitaji ya watoto wake wanafunzi shuleni, lakini kwa sasa anauwezo wa kutatua kila kinachohitajika katika familia yake.

Mnufaika Milembe Kipoya alisema, alianza kupata Sh. 44,000 tangu mwaka 2015 na mpaka sasa anapokea Sh. 46,000 fedha ambazo anazielekeza kununua vifaa vya shule vya wanafunzi, kukodisha shamba kwa ajili ya kilimo na kufanya mahitaji ya nyumbani.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Shibutwe Elikana Bunzali, alisema wanashirikiana na watendaji wa kata, vijiji na waratibu wa TASAF kuhakikisha wanufaika wote wanazitumia fedha katika shughuli muhimu za kuwaingizia kipato ili wasiendelee kuwa tegemezi hapo baadaye.

Vilevile, alisema mnufaika anayebainika kuzitumia fedha za mpango huo kinyume na utaratibu anahakikisha anamwajibisha kisheria kwa kumripoti kwa mtendaji wa kata kwa ajili ya hatua zaidi ikiwamo kumsihi na kumpatia elimu ya ujasiriamali ambayo ndiyo silaha yao ya kila siku.

Naye Mtendaji wa Kata ya Buzigonzi, Joseph Bahati alisema, awali wanufaika wengi walikuwa wakipokea fedha na kuzielekeza katika matumizi ya unywaji wa pombe, lakini baada ya kuanza kuwafuatilia na kuwapatia elimu ya ujasiriamali kila mnufaika anashughuli ya kumwingizia kipato.

HABARI ZA MAONYESHO YA NANENANE

# Serikali yaimarisha mfumo wa utoaji ruzuku mbolea

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

MKURUGENZI Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Stephan Ngailo, amesema serikali imeimarisha mfumo wa utoaji mbolea ya ruzuku kwa wakulima kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo ili kuziba mianya ya ubadhirifu.

Alisema Agosti 15 na 16, mwaka huu wanatarajia kutangaza tenda ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

Akizungumza katika maonyesho ya Nanenane kitaifa jijini hapo, Dk. Ngailo alisema hatua hiyo inalenga kuondoa kero, zilizojitokeza katika mifumo ya ruzuku iliyopita.

"Serikali imeandaa mfumo wa kielektroniki ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa kuziba mianya ya ubadhirifu hivyo wasambazaji wasitarajie kupata chochote," alisema Dk. Ngailo. Alifafanua kuwa ili kuhakikisha wakulima wananufaika serikali imejiwekea mfumo imara na bora ya utoaji wa ruzuku za mbolea ambao utasaidia kuwafikia wakulima.

Hata hivyo Dk. Ngailo alisisitiza kuwa katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika mifumo ya ruzuku iliyopita, serikali imejipanga vyema kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati sahihi.

Alisisitiza kuwa wakulima wanapaswa kujitoleza kujisajili kwenye mfumo huo, ili waweze kupata mbolea hiyo ya ruzuku.

Alisema lengo la kufanya usajili wa waingizaji, wasambazaji, wauzaji wa mbolea pamoja na wakulima ni kutaka wote kunufaika na mbolea hizo za ruzuku.

Alisema kuwa, mfumo huo utatumika kuhakikisha huduma zote za usambazaji wa mbolea za ruzuku unatolewa na mtu sahihi na kumfikia mkulima mwenyewe na si vinginevyo.

"Serikali imejipanga kuhakikisha mfumo huo unafanya kazi kwa ufasaha ili mkulima aweze kunufaika na ruzuku ya mbolea ambayo inatolewa," alisema Dk. Ngailo.

Akizungumzia namna usajili utakavyofanyika, Dk. Ngailo alisema usajili utafanywa na maofisa ugani walioko katika ngazi za kata na vijiji na kuthibitishwa na mwenyekiti wa kijiji na baadaye taarifa za mkulima kuingizwa katika mfumo wa kielektroniki ili kuwezesha usambazaji wa mbolea hizo.

Hata hivyo, alisema mzalishaji au mwingizaji wa mbolea nchini atatumia mifuko maalum kwa ajili ya ruzuku yenye QR code na maandishi yanayosomeka ruzuku ili kuutambulisha kuwa mbolea hiyo inanunuliwa na mkulima kwa bei ya ruzuku.

Alisema utoaji wa ruzuku za mbolea ni matokeo ya maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kuona umuhimu wa kuwawezesha wakulima kulima kwa tija na kufanya uhakika wa mavuno ya chakula na biashara kwa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

Sh. bilioni 150 zimetengwa ili kutumika kutoa mbolea za ruzuku kwa wakulima kwa mwaka wa fedha 2022/2023.



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, Mbaraka Batenga (wa pili kulia), akimsikiliza meneja wa kampuni ya kuuza dawa za mifugo na pembejeo za kilimo ya FARMBASE tawi la Arusha, Yahaya Kassim Saidi, kuhusu ubora wa viuatilifu, kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane, Kanda ya Kaskazini, jijini Arusha juzi. **PICHA GIFT THADEY**

# TOSCI yawataka wakulima kununua mbegu zenye lebo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI ya kudhibiti ubora wa mbegu Tanzania (TOSCI), imewataka wakulima kununua mbegu zilizokidhi ubora zenye lebo mpya ya kielektroniki ikithibitisha imekaguliwa.

Mkaguzi wa Ubora wa Mbegu TOSCI, Florence Kaaya, alisema hayo jana katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere wakati maonesho ya siku ya wakulima Nanenane Kanda ya Mashariki yanayojumuisha mikoa ya Pwani, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam.

Alisema mkulima anapaswa kuelimika kupitia banda hilo na kuhakikisha akifika dukani ananunua mbegu hasa za mazao ya chakula kwa kuhakikisha zina lebo ya TOSCI ili kuthibitisha ubora wake.

Kwa mujibu wa Kaaya, TOSCI ipo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kusimamia mbegu kuanzia hatua za mwanzo, ikiwamo kuhakikisha uhalisia wa sifa za mbegu mpya, kukagua mashamba ya mbegu, kupima ubora wa mbegu kwenye maabara zao na ukaguzi wa maghala.

Kaaya alisema TOSCI hujihusisha kuanzia mbegu ikiwa kwa mtafiti na kukagua kuona kama mbegu wanazozalisha ni bora, ili baadaye kampuni kubwa za mbegu zikiwamo Seed-co na ASA ziweze kuzalisha mbegu bora na kumfikia mkulima.

Alisema kampuni ya mbegu husimamiwa kuhakikisha wanatoa mbegu bora tangu wanapofanya ugunduzi, wanavyoipeleka shambani mbegu hiyo hukaguliwa kama kweli eneo wanapofanyia utafiti wao ni sehemu bora kwa ajili ya wakulima kupata iliyo bora.

Aidha, alisema wanakagua hadi inapofika kwenye mavuno na baadaye kutoa mafunzo kwa kampuni ya mbegu ya jinsi ya kupata bora na kufuatiliwa shambani.

"Kampuni kwenye utafiti ikishatoa mbegu italeta kwetu maombi ya kupimiwa usafi wa mbegu, uotaji na afya ya mbegu kama ina wadudu au nini na pia tunawasaidia kuwapa lebo ya TOSCI inayomfanya mkulima akienda dukani akikuta lebo hiyo kwenye mbegu anaamini kuwa ni bora kabisa na imehakikiwa na TOSCI," alisema Kaaya.

Aliitaka TOSCI kuhakikisha inaangalia usafi wa mbegu zinazotoka kwenye kampuni au shambani kama haina madhara yakiwamo magugu ambayo ni haribifu kwa mkulima yatailazimu TOSCI kuiondoa mbegu yote.

Alisema inatakiwa kuhakikisha haiendi kwa mkulima na kuyataja magugu hayo kuwa ni mabaya kama vile bangi na mengine zaidi ya aina tano mpaka 10.

Pia alisema huangalia uotaji wa mbegu kama itaota ikipelekwa kwa mkulima itamsaidia kulingana na mahitaji yake na kutoaa mfano wa mbegu ya mahindi ambayo huangaliwa viwango vya mahindi kwa kutumia maabara zao zilizothibitishwa kimataifa ambazo zina viwango vya uotaji kulingana na makubaliano ya kimataifa.

Kaaya alisema mbegu ya mahindi ya mtafiti au kampuni inatakiwa iote kuanzia asilimia 90 na ikiota kwa asilimia 70 kwenda chini itakuwa imepoteza sifa na kuiondoa.

Alisema mbegu ikiwa bora huipeleka kwenye maabara nyingine ya kuangalia afya yake ikikutwa na fangasi au virusi haitapitishwa, lakini ikiwa haina shida mhusika atapewa cheti cha ufaulu kwenye mbegu husika na kumruhusu kuomba maombi ya kupata lebo za TOSCI.

Naye Mkaguzi wa mbegu wa TOSCI, Zawadi Mwaikonyole, alisema matumizi ya lebo za kufuta yamesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti wauzaji wa mbegu feki wanaopaki mazao ya vyakula kama mbegu na kuwauzia wakulima.

Alisema lebo mpya za kufuta zilizoanza tangu mwaka 2020 zimesaidia kuondoa ufujaji huo kwa sababu zipo katika mfumo wa kielektroniki ambazo zinapaswa kusoma namba zake kwenye mfumo.

# Taasisi zaagizwa kusaidia wakulima, wafugaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Mashimba Ndaki, ameziagiza Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) na Taasisi ya Uzalishaji na Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kushirikiana kubuni teknolojia zitakazowasaidia wakulima na wafugaji kuongeza mnyororo wa thamani kupitia wanachozalisha.

Aidha, aliziagiza halmashauri kuweka mipango madhubuti itayowasaidia wajasiriamali kufanikisha biashara zao kupitia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa, pamoja na kuwaunganisha kwenye taasisi za kifedha wapate mitaji mikubwa itayowasaidia kukuza biashara zao.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao cha majumuisho baada ya kutembelea na kukagua mabanda mbalimbali yaliyoko kwenye maonesho ya wakulima Nanenane viwanja vya John Mwakangale jijini hapo.

Alisema wakulima, wafugaji na wavuvi wanakabiliwa na vikwazo kwenye shughuli zao kutokana na kukosa elimu sahihi ya kusimamia na kuendesha kazi zao, ukosefu wa masoko na mitaji.

Alisema taasisi zinazohusika na mnyororo wa thamani wa bidhaa hizo zitakapoungana na kuandaa mkakati wa kulisaidia kundi hilo itasaidia kuongeza uzalishaji na kufungua fursa za uwekezaji na masoko.

"Naziagiza taasisi zote za mifugo, kilimo na uvuvi kuunda mpango mkakati utakaojikita kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi, ili kupata tija na faida kupitia shughuli zao kuliko ilivyo sasa ambapo wanatumia nguvu kubwa kwenye kuzalisha, lakini hawapati faida vilevile halmashauri zote kuwaunganisha wajasiriamali na taasisi za kifedha ili kupata mitaji itakayowasaidia kukuza biashara zao," alisema Dk. Mashimba.

"Nimetembelea mabanda mengi ya wajasiriamali nimefurahi na kuridhishwa na ubunifu wao, lakini nimeona wanakabiliwa na tatizo la mitaji pamoja na vifungashio vizuri ambavyo vinaweza kuvutia biashara zao muhimu sasa tuwasaidia watu hawa."

Miongoni mwa wajasiriamali waliotembelewa na Waziri Dk. Mashimba, walisema vikwazo wanavyokabiliana navyo ni ukosefu wa mitaji, ili kukuza biashara na kuiomba serikali na wadau wengine kuwasaidia.

ama
ALHAMISI AGOSTI 4, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Simulizi ya ugumu kupatikana maji safi na salama inavyoumiza kichwa**



**Moto na mafuriko: Wataalamu wa dunia wanapohitaji kurudi darasani**

Ukurasa 14

# Vita mimba vyaivutia UNFPA nchini, yaahidi kusaidia 'mpaka kieleweke'

## • Yatoa mamilioni dola kununua vifaa

**Na Yasmine Protace**

UZAZI salama na wa mpango katika kanuni ya afya, inatoa mwongozo kumwezesha mtu kupata watoto aliyokusudia akiwa katika afya salama, pia ukisaidia haki ya kuamua wakati sahihi wa kuwa na mtoto.

Hivi karibuni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) limeahidi wanawake, wanaume na vijana kupata bidhaa muhimu za uzazi, pasipo kumuacha mtu nyuma.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA nchini, Mark Bryan Schreinerambaye, anasema katika kutimiza malengo hayo, wamenunua vifaa vya afya ya uzazi wenye thamani Dola za Kimarekani milioni 4.6 mwaka huu.

Katika hafla ya makabidhiano ya vifaa vya uzazi wa mpango, pia uzinduzi wa Ripoti ya Hali ya Idadi ya Watu Duniani, anawataja wachangiaji ni; ofisi ya UNFPA ugavi inayotoa zaidi ya dola 500,000 na kiasi kilichobaki kinatoka katika Ofisi ya Maendeleo ya Kimataifa na Juumuiya ya Madola, Uingereza (FCDO).

Anasema vifaa vya afya ya uzazi vilivyokabidhiwa na UNFPA nchini, ni vya kuokoa maisha ya uzazi, vikiwamo vifaa vya kisasa vya uzazi wa mpango.

"Bidhaa hizi ni za watu binafsi kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya afya zao za uzazi pindi na wakati sahihi wa kupata watoto," anasema Mark Bryan.

Anaongeza, vifaa hivyo vinàtoà njia ya uwezeshaji binafsi na hasa kinamama na wasichana, akiongeza lengo lao ni kusambaza dawa za uzazi wa mpango na vifaa vya afya ya uzazi kwa maelfu ya vituo vya afya, hospitali, zahanati na huduma za kijamii.

Mkuu huyo wa UNFPA anaelekeza pongezi kwa serikali nchini, dhamira ikiwa ni kuendeleza uzazi wa mpango unaozingatia haki, hata kubeba sifa sahihi ya kupata fedha za Kitanzania, shilingi bilioni 14 kwa ajili ya kudhibiti mimba.

Mark Bryan anaahidi kushirikiana zaidi na serikali ya Tanzania, dhamira yao ni kutanua wigo wa ufadhili hata baadaye.

Ni ahadi inayoendana na rekodi mwaka 2015, UNFPA nchini ilinunua asilimia 53 ya bidhaa za afya ya uzazi zilizokuwapo, thamani ya bidhaa hizo kwa jumla zikiwa Dola za Kimarekani milioni 52.2.

Anaongeza kuwa, bidhaa hizo zilitoa vidhibiti mimba vya kutosha vya kisasa, hata kutosheleza mahitaji ya wanandoa milioni 21 kwa mwaka mzima.

"Tunatarajia vifaa hivyo vitapunguza mimba zisizotarajiwa milioni tisa, kuzuia vifo vya karibu milioni moja vya uzazi, kuzuia utoaji mimba usio salama milioni mbili na kuokoa Dola za Marekani milioni 756 katika huduma ya moja kwa moja ya afya," anasema.

Anasema UNFPA inadumisha dhamira ya kuendelea na kuiunga mkono serikali, kupitia Wizara ya Afya kukabiliana na mahitaji ya afya ya jinsia na uzazi na hasa ya wanawake na wasichana.

Kwa mujibu wa Mark Bryan, juhudi hizo ni pamoja na kuimarisha mfumo wa ugavi na manunuzi, kuinua uwezo watoa huduma wa afya ya uzazi, mama, vichanga, watoto na vijana.



Sanaa ya maonyesho ikitumika kudhibiti mimba za utotoni. **PICHA: MTANDAO**

Anasema umuhimu wa upatikanaji wa vidhibiti mimba umeainishwa katika Ripoti ya Idadi ya Watu Duniani ya UNFPA, iliyozinduliwa mwaka huu ikiwa na jina "kuona yasiyoonekana".

Mkurugenzi Mtendaji wa UNFPA, Dk. Natalia Kanem, anasema Utafiti wa Demografia ya Afya Tanzania ya mwaka 2010, ilikadiria asilimia 26 ya watoto waliozaliwa katika kipindi cha miaka mitano kabla ya utafiti, wanatokana na mimba zisizotarajiwa, hasa vijana wenye ufahamu mdogo wa upangaji uzazi, pia uhaba wa vifaa vya kuzuia mimba.

"Asilimia kubwa ya vituo vya afya vya umma nchini Tanzania ambavyo vinakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya uzazi wa mpango, vinaonyesha kutokidhi mahitaji ya upangaji uzazi," anaongeza.

Dk. Kanem anasema, UNFPA inaiunga mkono serikali kwa kutimiza ahadi ya Mkutano Mkuu wa Nairobi mwaka 2019 wa kusaidia upatikanaji wa afya ya uzazi, watoto wachanga na vijana.

Anaongeza kwamba wanalenga kuhakikisha hakuna jamii inayoachwa nyuma katika hulo, wakiwamo wenye ulemavu, wakimbizi na wale walio hatarini zaidi, dira kuu ni mageuzi ya kufuta mimba zinazozuilika.

**MRATIBU AFYA**

Dk. Felix Bundala, Mratibu wa Afya ya Mtoto kutoka Wizara ya Afya, akiongoza pia Kitengo cha afya ya Uzazi, anaipongeza UNFPA kwa kuwapatia msaada huo, akihdi uwawafikia walengwa wote kitaifa, akitaja mkakati walio nao ni kupunguza vifo vya uzazi na watoto wachanga na walio chini ya miaka mitano.

MAZINGIRA

# Simulizi ya ugumu kupatikana maji safi na salama inavyoumiza kichwa

- Watoa huduma, watumiaji, waratibu...
- Wabeba ndoo safari ndefu wafunguka yao

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KUKOSEKANA majisafi na salama katika sehemu mbalimbali na hasa vijijini kunaibua vilio vingi, ndani ya kaulimbiu yenye heshima 'Maji ni Uhai.'

Zao lake ni watu wanaendelea kutumia maji ya madimbwi na visimani, yasiyo safi na salama, ikiishia kuibuka magonjwa ya mlipuko, mbadala wake, ni watu wakitembea umbali mrefu, kusaka majisafi.

Asilimia kubwa ya magonjwa hayo yamekuwa yakiwapata watoto wadogo ikilinganishwa na watu wazima. Katika kutatua hilo, serikali imeunda chombo mahususi cha kutatua kero ya ukosefu wa maji vijijini, RUWASA, lakini bado kuna maeneo hayajatatua shida hiyo.

Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019, inaipa RUWASA jukumu la kuhakikisha wananchi waishio vijijini nchini wanapata huduma ya majisafi na salama ikiwa ni sehemu ya 'kumtua mama ndoo kichwani.'

Nayo Sera ya Maji ya Taifa ya Mwaka 2002, inarejea huduma ya maji ni bidhaa inayohitaji uwekezaji na utunzaji wa mazingira ya vyanzo vya maji, kwa kupata miti rafiki, ili huduma hiyo iendelee na kuwa na maji ya kutosha.

Ni sera inayotoa mwongozo wa kuwapatia wananchi maji safi na salama kwa umbali usiozidi mita 400. Hata hivyo, ikirejewa uhalisia uliopo bado hali ni tofauti, kwamba wananchi wanatembea umbali mrefu kusaka huduma hiyo na ndio umekuwa mwanzo wa madhara kama ya fisi.

Kwa ukubwa uliopo wa uhaba wa maji vijijini, RUWASA imekutana na kufanya majadiliano na vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii kwa lengo la kuelewana, kutathmini na kubadilishana uzoefu unaohusu maji safi, ili kuhakikisha vyanzo vyake vinatunzwa, vikiwa na mazingira safi yenye miti rafiki.

**KINACHOJIRI KAHAMA**

Kimsingi, haki hizo zinazoangaliwa kisera na kisheria, bado zinaangukia vitendawili, hasa wilayani Kahama mkoa wa Shinyanga, ambako Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, Flora Sagasaga, anasema kuna maeneo bado kunatumika kisima kimoja kwa watu na mifugo yao.

Ni kutokana na hali hiyo, anaeleza rai kwa serikali kuweka nguvu vijijini, ambapo anakutaja kukabiliwa na ukosefu mkubwa na huduma ya maji safi na salama.



Hayati Rais Dk. John Magufuli, alipozindua mradi mkubwa wa maji katika Kata ya Kakola wilayani Kahama. **PICHA: MTANDAO**

"Magonjwa ya mlipuko yanayotokana na utumiaji wa maji machafu. Hayataweza kwisha, kwa sababu bado wananchi wetu wanaendelea kutumia maji na wanyama, hivyo tujielekeze katika kuchimba angalau visima virefu vya maji vijijini," anasisitiza Flora.

Katika hoja hiyo, Diwani wa Ngogwa katika halmashauri hiyo, Kamuli Mayunga, anasema kuna mradi wa maji umekamilika kwenye kata yake, lakini analalamika haujaanza kutoa huduma kwa umma.

Anasema, ni hali inayosababisha wananchi kuendelea kutembea umbali mrefu kutafuta maji, hata kutolewa mikasa ya watu kujeruhiwa na wanyama wakali, akataja mojawapo mnyama fisi.

Thomas Muyonga, kiongozi wa kisiasa aliyeko Ngogwa, anaungana na Diwani Mayunga, akisema uhitaji wa maji hasa vijijini bado ni makubwa, licha ya serikali kuelekeza nguvu kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama ya uhakika.

Mkazi wa Kata ya Ngogwa, Agness Mussa anatoa ushuhuda kwamba, wamekuwa wakiamka alfajiri kwenda kutafuta maji na wanakutana na fisi ambao tayari wako katika historia ya kudhuriwa kwa namna mbalimbali, hata akashinikiza rai yake kutaka mradi uanze kazi haraka.

**MENEJA RUWASA**

Mhandisi Maduhu Magili, Meneja wa RUWASA Kahama, anasema wamekuwa wakitatua tatizo la ukosefu wa maji kwa wananchi, kupitia uanzishaji miradi mbalimbali ya maji, ikiwemo visima vilivyokufa kwa kuvifanyia marekebisho vianze kutoa huduma tena.

Anasema, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, RUWASA wilaya ya Kahama, ilipanga kutekeleza miradi ipatayo 26 katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa Kahama, miradi mitano ya kukamilisha na 21 mipya.

Magili anaifafanua miradi hiyo, ni ile inayotafutiwa vyanzo vipya vya maji na kutengewa bajeti ya kiasi cha Sh. bilioni 8.842 na hadi kufika Mwezi Aprili 30, mwaka huu fedha zilizotolewa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni kiasi cha Sh. bilioni 6.685 sawa na asilimia 75.6.

Anafafanua, kuna miradi 21 mipya na mitano inayorekebishwa, kati yake mitatu imeshakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi na miradi miwili inaelekea na marekebisho ambayo inakwenda kukamilika hivi karibuni.

Anasema, huduma za maji katika maeneo ya vijijini husimamiwa na kuendeshwa na Jumuiya za Usimamizi wa Huduma za Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO), lakini mingi inakufa baada ya kukosa usimamizi madhubuti na wahusika kushindwa kukusanya ankara ipasavyo.

ANAANIKA CHANGAMOTO

Magili anataja changamoto zilizopo kwa wasimamizi wa maji ni ufinyu wa bajeti na ukosefu wa vyanzo vya maji vya uhakika kwenye baadhi ya maeneo, hususani maeneo katika Halmashauri ya Ushetu.

Analalamika kuwepo hali duni ya miundombinu na hasa mitambo kuchakaa katika mitandao ya mabomba kwenye miradi ya zamani.

Kiongozi huyo anasema, upatikanaji majisafi na salama kwa eneo analosimamia ni wastani wa asilimia 66, sawa na watu wanaohudumiwa 490,813 ya wakazi wote 742,521 waliopo vijijini.

Hata hivyo, anatoa ahadi kwamba baada ya kukamilika mradi unaojengwa, kiwango cha upatikanaji majisafi na salama kinatarajiwa kupanda hadi asilimia 74.6 ifikapo Machi mwaka ujao.

**BONDE TANGANYIKA**

Mhandisi Odemba Kornel, ni Mkuu wa Utunzaji wa Vyanzo vya Maji Bonde Ziwa Tanganyika, anasema wamekuwa wakifanya tafiti kuwepo maji kabla ya ujenzi wa miradi, ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji ya kutosha katika eneo la mradi, lengo ni kunufaisha watumiaji.

Anasema maeneo mengi vijijini, miradi ya maji inakauka baada ya wananchi kuanzisha shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji, kupanda miti isiyo rafiki na vyanzo hivyo. Hapo anawataka wavitunze vyanzo hivyo kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Wakala wa Vipimo Mkoa wa Shinyanga, Leo Patrick, anasema kuwepo malalamiko ya kupanda ankara za maji kwa watumiaji, kunasababishwa na kutokukaguliwa kwa dira za maji (mita) na Wakala wa Vipimo (WMA), hali anayoitaja inasababisha wateja waendelee kulipa gharama kubwa, isiyofanana na matumizi yao .

Anasema, ili kuondoa tatizo hilo kwa wananchi, wameanza kukagua dira za maji na kutoa elimu kwa wateja kwa kuanza na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) na kuziweka siri kuonyesha kama zimekaguliwa hali ambayo sasa imepunguza malalamiko kwa baadhi ya wateja.

Patrick anadai, baada ya kuhitimisha zoezi la ukaguzi wa dira hizo watajielekeza katika Mamlaka ya Maji Kahama (KUWASA) na lengo la kufanya zoezi hilo ni kuondoa malalamiko kwa watumiaji na kuhakikisha kila mteja analipa ankara kwa anachokitumia.



Mkuu wa Utunzaji wa Vyanzo vya Maji Bonde la Ziwa Tanganyika, Mhandisi Odemba Kornel, akieleza namna wanavyotunza vyanzo vya maji na mazingira yake, kuhakikisha maji yanapatikana **PICHA: SHABAN NJIA**

AFYA

# Namna afya bora ya mtoto, mzizi wake wazazi wamleavyo pamoja

## • Wenye ukweli waja na ushuhuda

**Na Rausath Sued, SJMC**



Ofisa Ustawi wa Jamii katika Jiji la Dodoma, Heriely Kutwama, akitoa elimu kwa kundi la watoto waliotembelea Banda la Maonyesho ya Idara ya Afya.

KATIKA maisha mwenendo wa jamii hasa inapoishi pamoja kifamilia ikiwamo mke na mume, mtoto anaangukia kada ya kulelewa.

Muhimu ni kusimamia usalama na ustawi wake, ili kumnufaisha mtu huyo na baadhi ya mambo yahusuyo afya yake.

Ni aina ya majumuisho yanayomgusa kwa kipindi kilichoko na kijacho, tafsiri kuu ya mwongozo ikiangukia dhana kutoka Sheria ya Haki za Mtoto ya Mwaka 2009 inayotamka: "Mtoto ni mtu yeyote aliye na umri chini ya miaka 18."

Ndani ya mandhari hayo ya kijamii na kisheria yanayoanika tafsiri na ulazima wa wazazi kumlea mtoto pamoja, kunaibuka mjadala mkubwa katika jamii ya Kitanzania yenye swali "ni nani anayewajibika na malezi hayo?"

Katika kurejea kiulizo cha kumtambua mwenye jukumu la malezi ya mtoto, wengi wanaamini kuwa mama ndiye anayebeba jukumu zima la malezi hayo ambayo daima kipengele cha afya yake ni 'chanda na pete.'

Mara zote mama anatajwa kuwa moja ya nguzo muhimu sana katika jamii na hata familia, pia ndiye mlezi wa familia, huku upande wa pili wa shilingi, baba naye ana mchango mkubwa katika malezi ya watoto kwa kuegemea usemi wa wahenga 'baba ni kichwa cha familia.'

Hata hivyo, katika uhalisia wa kinachojiri hivi sasa ndani ya jamii kuna sura mpya inayojitokeza kuibua uhalisia mpya. Ni jukumu linaloibuka tofauti na kilichozoeleka, hivyo kuleta maswali mengi kuhusu nani hasa mwenye jukumu katika malezi ya mtoto?

Hapo Sheria ya Haki za Mtoto ya Mwaka 2009 inataja baadhi ya haki ni ya mtoto kuishi na wazazi wake. Swali lililopo, je hilo linatekelezwa?

Joyce Maketa, ni Ofisa Ustawi wa Jamii, kutoka Manispaa ya Ilala anayeeleza:"Sheria ya mtoto katika malezi inatamka ni wajibu kwa wazazi wote wawili kushiriki na kuwa na jukumu la malezi imara kwa mtoto, japo kwa nchi yetu hili swala limekuwa tofauti, ila baba na mama inabidi wachukue jukumu la malezi kwa mtoto."

**HALI INAYOJIRI**

Ikirejewa Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania ya Mwaka 2008, inatamka ulinzi wa mtoto unapaswa kuanza hatua za ukuaji mtoto na baada ya kuzaliwa. Je, hilo linafuatwa?

Nchini Tanzania kuna matukio yanayohusisha wazazi wa kiume kuwatelekezea wenza wa kike jukumu la kulea na kuhudumia watoto.

Hapo mwanamama, Consolatha (jina la pili tunalo) mkazi wa Mbezi Beach, Dar es Salaam, ana ushuhuda anaofafanua kwamba hadi sasa analea mtoto peke yake, akikumbana na changamoto nyingi katika malezi hayo.

"Kumlea mtoto ukiwa peke yako ni changamoto, kwa sababu mtoto anakosa malezi ya wazazi wote na mtoto anapokosa malezi ya baba, lazima kuwepo tofauti.

"Kuna muda mwanangu anahitaji kumjua baba yake, kuna muda nagombana na baba yake kwa sababu ya matumizi, yaani changamoto kibao tu," anaeleza Consolatha.

Hadi sasa kuna malalamiko mengi yanatajwa ya kutambua umuhimu wa baba na mama katika malezi ya mtoto, kwamba kinamama wengi nchini wanashindwa kuripoti matukio aina hiyo kwenye mamlaka husika hata wakaweza kupata msaada kisheria, kutokana na sababu mbalimbali.

Cosolatha analifafanua hilo: "Mimi inaniwia vigumu kuripoti hili suala, kwa sababu nawaza vipi mwanangu akija kujua na kusikia kuwa baba na mama wanashitakiana. Haitokuwa vizuri na itamuathiri mtoto. Kwa hiyo, ndio maana niliona bora niache tu kwa ajili ya maisha ya mwanangu."

Mfanyabiashara Richard Sylvester, mkazi wa Mikocheni, Dar es Salaam ni baba katika, familia, anayeeleza maoni yake kwamba jukumu la kumlea mtoto na kumhudumia ni la wawili, yaani baba na mama

"Mimi kama baba naamini mtoto anahitaji malezi ya wazazi wote wawili. Mtoto kupata malezi ya mzazi mmoja anakosa mengi, hivyo wazazi tujitahidi kuwa wamoja ili watoto wapate malezi bora," anasema.

Richard anasisitiza: "Wazazi wa kiume inabidi tuwe makini katika hili suala kwa sababu kama ukiamua kupata mtoto basi uwe umejipanga kuchukua jukumu la kulea kama baba. Hivyo basi, wazazi wa kiume tubadilike, tuwape watoto wetu malezi mazuri."

Anafafanua kwamba ni hali inayowagusa zaidi watoto, kwani ndio walio katika mahitaji zaidi ya malezi kutoka kwa baba na mama. Hapo kuna ushuhuda wa kuwapo simulizi za ushahidi wa mateso kutoka kwa binti Matia (jina la pili tunalo), mwenye umri wa miaka 14.

Huyo ni mwanafunzi wa shule moja ya sekondari katika wilaya ya Kinondoni, akiwa na simulizi ndefu kuhusu athari anazozipata kwa kulelewa na mama, akitamka:

"Mimi tangu nimezaliwa baba simjui. Nimelelewa na mama na mpaka hapa anayenisomesha ni mama. Hii inanipa fedheha kwa sababu muda mwingine naondolewa shule kwa sababu ya ada," anasema.

Katika hilo, Joyce Msivule, mwanzilishi wa kituo cha kulea watoto kilichopo Tandika, Dar es Salaam, ana ufafanuzi wake: "Katika vituo vya kulea watoto takriban asilimia fulani ya watoto ni wanaolelewa na mzazi mmoja hasa mama na matokeo yake, mama anashindwa anaamua kumleta mtoto kituoni."

Kiiya Kiiya, ni Mtendaji Mkuu wa shirika la C-sema lenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam, anasema wako katika shirika linalofanya ulinzi wa sheria za mtoto kupitia mradi wake wa huduma ya simu, kwa mtoto ulioanzishwa mwaka 2013.

"Kwa mujibu wa ripoti tulizo nazo rasmi na zisizo rasmi ni kwamba, vitendo vingi vya kikatili vinatoka kwa watu wa karibu wa mtoto kama vile wajomba na baba.

" Si kama wanavyodhani watu wengine kwamba vinatoka kwa watu wa nje kama bodaboda. Vitendo hivyo vya kikatili, ni pamoja na mzazi mmoja au wote wawili kumtelekeza mtoto" Kiiya anasema.

Kwa mujibu wa asasi hiyo ya C-sema, mtoto akiwa salama dhidi ya vitendo hivyo dhalimu, kuna uwezekano mkubwa wa kukua na kuendelea vizuri kiafya, usalama na kisaikolojia kuwa mtu mwema na muwajibikaji kwenye jamii.

Katika hilo, ndipo Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania ya Mwaka 2008, inahimiza ulinzi unaoenda sambamba na hatua zake za ukuaji.




Tukio lenye tafsiri pana kwa afya na usalama wa watoto. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MAZINGIRA

# Moto na mafuriko: Wataalamu wa dunia wanapohitaji kurudi darasani



Joto la kupindukia nchini Uingereza, hata wakazi wake wanakimbilia ufukweni kutafuta nafuu.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

MIJADALA kuhusu mabadiliko ya tabianchi imekuwapo kwa karibu nusu karne, ikiwa ni mchepuo wa wimbi la kiitikadi dhidi ya silaha za nyuklia, baada ya Japan kupigwa mabomu mawili ya atomiki mwaka 1945.

Sehemu ya wanaharakati ikafikia na hoja kuwa tatizo hasa ni mwelekeo wa uchumi wa viwanda, kwani unaharibu uasilia wa binadamu na kusababisha majanga katika afya na mazingira.

Hatua moja baada ya nyingine, ikagundulika kuwa kuongezeka kwa viwanda kunaongeza joto na kutoboa tabaka la ozoni angani, hali inayoruhusu mionzi isiyochujwa ya jua kuivuruga sayari wanayoishi wanadamu.

Ikiangaliwa kwa vipengele, kile kinachojadiliwa katika kurasa za kitaaluma za mitandao, inapatikana picha, kuwapo wimbi la kutaka kuelewa na hata kujifunza, kinachotokea sasa.

Ila msingi wa jitihada hizo ni kile kinachofahamika kwa wataalamu, yaani itikadi kongwe za tabianchi ambazo zinatofautisha mielekeo ya kiliberali kwa upande mmoja na kihafidhina kwa upande mwingine.

Maoni ya kila mtaalamu ni kielelezo cha undani wake katika mwelekeo wa namna mbalimbali, mfano 'mliberali poa' ambaye hakasirishwi na uchumi wa viwanda, au kuna mhafidhina 'siasa kali' asiyetaka kusikia mijadala ya tabia nchi na si kitambo sana mijadala ya corona.

Kuna mchepuo wa majadiliano umetungiwa kichwa maalum 'floodafterfire' yaani mafuriko, baada ya wingi wa moto, kwani eneo moja likiungua hasa kama ni vilima linakosa kabisa uwezo wa kusitiri maji mvua ikinyesha.

Wakati huohuo, ongezeko la joto duniani linaelezwa kuchangia kuyeyuka mabonge makubwa ya barafu katika ncha za dunia na kuongezeka usawa wa maji baharini, kunapochochea kuinuka uwezo wa vimbunga na kusomba maji kwa mawimbi ya kutisha kuelekea fukwe hasa maeneo ya mashariki ya mabara makuu. Sehemu isiyo ndogo ya mafuriko inatoka huko, halafu mvua kubwa.

### DUNIA INAKOELEKEA

Andiko la kitaalamu mtandaoni, linaonyesha watu pia huuliza: "Hivi tunaweza kutabiri moto wa nyika? Moto wa nyika unaongezeka?"

Kimsingi, swali la kwanza siyo rahisi kufafanuliwa, kwani siyo kila mahali kunalipuka moto nyikani, wakati joto la kiangazi likifikia viwango vya kushangaza hivi karibuni.

Wengi wanahofia kuwa mwezi Agosti utakuwa wa maafa ya kupitiliza, kwani mwezi uliopita umetawaliwa na balaa la viwango vya juu vya joto, hasa katika maeneo ya kaskazini ya dunia.

Ikirejewa, kuna anadiko la kisayansi linaloakinisha kuwa moto, ukame na mafuriko vinatabirika kisayansi, ambalo si geni, bali tangu mwaka 2006, Agosti, hali inayoashiria ushahidi sasa.

Tatizo linaonekana pale kunakuwapo hoja ya kujaribiwa kutafsiriwa hali ya namna hiyo, mtaalamu akifafanua kwamba, kuna wakati viwango vya joto vinaongezeka na kuna hali hatarishi ukipata majina ya kitaalamu; ikipata majina ya moto wa nyika, 'ukame na mafuriko yanayotabirika katika miaka 200 ijayo.

Hata hivyo, sura ya changamoto iliyoko ni kwamba hadi kufikia dira hiyo ya miaka 200 mbele ndani ya uchumi imara, maana yake ni kwamba ongezeko la joto, moto, ukame na mafuriko inapaswa kudhibitiwa.

Ukame nao unaweza kudhibitiwa, kwani athari yake kubwa zaidi ni katika kilimo ambacho kiinashika maisha ya umma; vivyo hivyo chemchemi za maji baridi na uwepo wa mito inayojaza maji baharini, huzuia bahari kudhoofu.

Kimazingira, pasipo maji kuingia baharini, uduni wa virutubisho vya maji baridi na hata hewa oksijeni inayotakiwa na samaki (pia wanyama wengineo ndani na nje ya maji), inakuwa hali hasi.

Ina maana kuwa, kupambana na ukame siyo tu suala la kutafuta maji chini ya ardhi au katika mito, ila kuendeleza kwa nguvu uoto katika maeneo kame ili kuongezea uwepo wa mvua na kuimarisha chemchemi hizo.

Wakati baadhi ya wataalamu wanazungumzia cha kufanya katika miaka 200 ijayo, wengi wanaona hata sasa kuna hali ya tahadhari kimazingira inayoendelea na kuingia viwango vya janga la tabianchi kwa haraka sana.

Moja ya nchi ambako halo limekuwa dhahiri ni Australia, ambako wataalamu wanaakinisha uhusiano wa karibu kati ya moto na mafuriko.

### MAONO YA KITAALAMU

Wachambuzi wa timu iitwayo 'National Public Radio' huko California nchini Marekani, wanasema hali ya baadaye ya dunia itakuwa sayari yenye joto zaidi, inayoashiria majanga zaidi ya tabianchi, kwani vimbunga, moto wa nyika na mvua kubwa za kushtukiza zinazosababisha mafuriko ya kutisha imeanza kuonekana.

Wataalamu wanaoshirikiana na gazeti la Uingereza la 'Financial Times' sasa wanakiri kuwa mabadiliko ya tabianchi yanaongezeka kwa haraka kuliko jinsi ilivyotazamiwa, kwa mujibu wa halio iliyofikiwa hadi sasa.

Kuongezeka joto na kuyeyuka mabonge makubwa ya barafu bahari ya Kaskazini ya dunia, Arctic (na hata Kusini, Antarctic) vimeongeza nguvu ya mawimbi ya bahari na mafuriko, zao la moto ukiwa na mchango mkubwa kwenye kasi ya mawimbi hayo ya maji.

Hitimisho la jumla la mazingira hayo, ni kwamba bado wataalamu hawajafikia mahali wanakotambua kwa pamoja makali ya janga linayoinyemelea dunia, huku kukikosekana mkakati wa pamoja wenye uwezo wa kukabiliana na hali hiyuo.

Kinachojadiliwa kwa nguvu ni malengo ya mkutano uliopita wa mabadiliko ya tabianchi duniani (COP 26) na uliofuata Novemba mwaka jana, jijini Glasgow Scotland (COP 27), ambayo kimsingi yanazungukia mkakati wa 'Net Zero'.

Hapo inalenga kulinganishaa utoaji hewa haribifu kwa shughuli za uchumi au wataalamu wanavayoiita 'shughuli za binadamu', hewa haribifu ipungue.

Inaelezwa, suala la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, inavuta ulazima wa kuisimamia Umoja wa Mataifa jukumu la dunia kuwa na mikakati toshelevu ya kuwekeza mbinu za kukabili moto, pia mazingira makubwa ya jangwa.

Hapo kunajenga hoja ya kuwapo mambo kama kusafisha maji ya bahari, kujenga maeneo mapya ya kuzuia maji kwa kuyakinga kupitia mabonde yaliyozibwa njia zake, yasisambae chini ya ardhi na si kutegemea mataifa kama Jamhuri ya Kidemokarasi ya Congo (DRC) na Brazil walinde misitu baki ya Congo na Amazoni, inayobatizwa 'mapafu ya dunia.'



Kikosi cha Zimamoto nchini Ufaransa, kikipambana kukabili mlipuko wa moto nchini humo, hivi karibuni.



## HABARI DODOMA

### Shekimweri awaonya wanaopotosha sensa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, ametaka wananchi kujiepusha na upotoshaji na mila potofu kuhusu sensa itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu sensa, Shekimweri alisema ni vyema watu wakatafakari na kujiuliza kwa kuwa sensa sio mara ya kwanza kufanyika nchini.

"Tujiulize je, ni mara ya kwanza sensa kufanyika? Je, kuna ambao walihesabiwa wakapata madhara yoyote? Katika sensa zote zilizotangulia hakuna ambaye alihesabiwa akajitokeza hadharani kwamba amepata madhara fulani, tujiepushe na upotoshaji, tuwabeze, tuwapuuze na tusiwafuate, sensa ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu tujitokeze kuhesabiwa," alisema.

Alisema kuna kila sababu ya wana Dodoma kushiriki ipasavyo kwenye sensa hiyo ili waendelee kunufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Kuna kazi kubwa imefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali kuu, kwa uchache ni kama barabara ya mzunguko, barabara za katikati ya jiji lakini ujenzi wa mji wa serikali, ujenzi wa mwendokasi, Uwanja wa Ndege Msalato na ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea cha Intracom."

"Kuna mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambapo Sh. bilioni 12 zimetolewa, ujenzi wa soko la wazi la Machinga, Sh. bilioni 9.4, tunaona kwa heshima ya Rais anayofanya kwa Jiji la Dodoma na bado tunauhitaji wa miradi mingine inahitajika Dodoma kwa ajili ya maendeleo ya wananchi."

"Ili serikali itekeleze haya yanayohitajika kwa Dodoma ni lazima kupata takwimu za watu wa kuzingatiwa kwenye miradi hiyo ni kwa sababu hiyo najitokeza hadharani kuwaomba wana Dodoma wote tuitikie rai ya Rais wetu tarehe 23 Agosti mwaka huu kila mwana Dodoma, wategemezi wake na wageni popote watakaokuwa wasafiri na wanaoamkia tarehe hiyo Dodoma na wazee na watu wenye ulemavu wahesabiwe," alisema.

Alisema ni muhimu kuhesabiwa ili kujua idadi ya wananchi wa Dodoma na Watanzania wapo wangapi.

"Sensa ni muhimu hutekelezwa kila baada ya miaka 10 nia ni kufahamu idadi ya watu ili tunapopanga mipango ya maendeleo na kutenga bajeti za kutekeleza ziwe na uhalisia na ziwe na idadi ya watu walioko, niwaombe sana kila mwananchi ahamasike na kila kiongozi wa mtaa, kata atufikishie ujumbe huu kwa watu anaowaongoza, wawe wa kisiasa, wa kidini, kimila, tuhamasishe watu wajitokeze," alisema.

# Dodoma kupokea lita mil. 130 za maji kutoka Mtera

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na kero ya mgawo wa maji ulioko hivi sasa jijini Dodoma, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kwa kushirikia na Wizara ya Maji imeanza mikakati ya kutoa maji lita milioni 130 kutoka Bwawa la Mtera.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alibainisha hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua na kujiridhisha kuwa chanzo hicho cha maji ambacho pia kinatumika katika kuzalisha nishati ya umeme.

Aweso alisema kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Kaimu Meneja wa kituo cha kufua umeme Mtera, chanzo hicho kitatumika kuzalisha lita hizo za maji ili kuondoa upungufu kwa sasa. "Tunawashukuru wenzetu wa TANESCO kwa ushirikiano waliotupatia kuhakikisha mpango huu unakwenda kutimia na kusaidia kukabili kero ya mgawo wa maji iliyoko hivi sasa katika Jiji la Dodoma kutokana na kukua kwa kasi pamoja na ongezeko la watu," alisema.

Alisema kutokana na Dodoma kukua kwa kasi mahitaji ya maji yanaongezeka kila siku na iko haja ya kutafuta vyanzo vingine vya uhakika.

"Hivi sasa Dodoma pamoja na ongezeko kubwa la watu, lakini mahitaji ya maji katika shughuli za ujenzi, viwanda yamekuwa makubwa sana hivyo wakati tunasubiri vyanzo vingine vikubwa kama Bwawa la Farkwa na Ziwa Victoria, lazima tuanze na huu kwanza kwani hakuna ziada mbaya," alisema Aweso.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema mahitaji ya maji kwa sasa katika Jiji la Dodoma ni takribani lita milioni 133 kwa siku.

"Kwa sasa tunao uwezo kwa kuzalisha kwa siku lita milioni 67 hivyo upungufu ni lita milioni 66, lakini kama tutafanikiwa mradi huu na kupeleka maji katika jiji la Dodoma kwa hizi lita milioni 130 tutakuwa na uwezo wa kuzalisha maji lita 201 kwa siku na kufanya kuwa na ziada kwa zaidi ya miaka 13," alisema Joseph.

Kaimu Meneja wa kituo cha kufua umeme Mtera, Moses Holela, alisema mpango huo wa kutoa kiasi hicho cha maji kwa siku hauwezi kuathiri shughuli za uzalishaji umeme.

"Bwawa letu lina uwezo wa kujaza maji lita trilioni 3.7 na sisi katika shughuli zetu za uzalishaji wa umeme tunahitaji lita 85,000 kwa sekunde na kwa mwaka ni lita milioni 2.6 hivyo kiasi kingi cha maji bado kinabaki, kama sasa ni wakati wa kiangazi, lakini bado yapo maji ya kutosha," alisisitiza Holela.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), akikagua Bwawa la Mtera, alipofika kujiridhisha kuhusu kina cha maji cha bwawa hilo, mkoani Dodoma juzi. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma, inatarajia kuanza mradi wa kuchukua maji kwenye bwawa hilo hadi Dodoma Mjini kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Vijana washirikishwe mipango ya maendeleo'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuwashirikisha vijana katika mipango ya maendeleo ili kuinua kundi hilo kiuchumi.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alitoa kauli hiyo jana jijini hapo alipokuwa akizindua ujenzi wa nyumba ya mshindi wa kwanza atakayepatikana katika mashindano ya mbio za waendesha pikipiki kitaifa yanayoratibiwa na Shirika la Global Peace Advocacy for Conflict Resolution kwa kushirikiana na Umoja wa Waendesha Pikipiki Mkoa wa Dodoma (UWAPIDO) yanayotarajiwa kuhitimishwa Agosti 30, mwaka huu.

Mashindano hayo yanayojulikana 'Tanzania Royal Tour Rally 2022' yanalengo la kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza fursa za utalii nchini kupitia filamu ya Royal Tour.

Shaka alisema CCM inaamini vijana wakiwezeshwa na kushirikishwa kiuchumi kupitia fursa mbalimbali wana uwezo wa kuchangia maendeleo ya taifa kwa kiwango kikubwa.

"Rais Samia ni mwongoza njia, mfungua fursa na ana maono ya kuwakomboa vijana kiuchumi kupitia fursa na rasilimali zilizoko nchini," alisema.

"Rais Samia amefungua mlango kupitia filamu hii ya kuonyesha fursa za kujitegemea kiuchumi kama ambavyo nyie mmefanya, lakini kuvutia watalii nchini ili kuongeza pato la taifa, hapa Dodoma kuna vivutio vya utalii vimewekewa mpango gani wa kutangazwa, nyie mnaweza kuwa mabalozi wazuri wa kutangaza utalii," alisema.

Shaka alisisitiza madereva pikipiki na bajaji wanapaswa kuungwa mkono kwa kuwafungulia fursa za ajira.

"Mmeonyesha mfano mzuri Halmashauri ya Jiji la Dodoma imewakopesha Sh. milioni 300 na hadi sasa mmerejesha zaidi ya Sh. milioni 200, asilimia 80 ya mkopo mmerejesha, mkijengewa uwezo na mkiandaliwa vizuri mtakuwa na mchango mzuri," alisema.

Aliwataka kuhamasishana kushiriki Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu pamoja na kuendelea kupata chanjo ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Global Peace Advocacy for Conflict Resolution, Ryamoja Mfuru, alisema taasisi hiyo imeandaa mashindano hayo kuwawezesha waendesha pikipiki kubeba ujumbe wa kuhamasisha utalii nchini.

Alisema mbio hizo ngazi ya wilaya zitaanza Agosti 13, mwaka huu na Agosti 17 zitaendelea kwa ngazi ya mkoa na kuhitimisha kitaifa Agosti 30 kwa mshindi kukabidhiwa nyumba.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya State Aviation, Amour Abdallah, alisema kampuni hiyo itatoa helikopta kuhamasisha tukio hilo kwa kuwa uwezeshaji vijana hususan madereva hao ni msaada muhimu wa kuchangia maendeleo ya taifa.





# Serikali kuzaliza ng'ombe 300,000 njia uhawilishaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema imepanga kuzalisha zaidi ya ng'ombe 300,000 kwa njia ya uhawilishaji ili kuongeza ubora wa mifugo na tija kwenye uzalishaji pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliyasema hayo jana jijini Mbeya alipokuwa anapokea dume la kisasa ambalo serikali imepewa na Kampuni ya Mbogo Ranches ya wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu.

Alisema ng'ombe watakaozalishwa kwa njia hiyo wana uwezo wa kutoa maziwa mengi kuliko wale wa kienyeji na kusisitiza wafugaji kuchangamkia aina hiyo ya ng'ombe na kuachana na wale wa kienyeji.

Alisema serikali inalenga kupunguza mifugo kuchungwa na kuhamasisha wafugaji kufuga mifugo ya ndani ili kupunguza migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji.

"Sisi kama serikali tunaliona tatizo mbele ambalo linaweza kutukabili la upungufu wa maeneo kwa ajili ya kuchungia, kwa hiyo tunawashukuru wenzetu wa Mbogo kwa kutupatia hili dume ambalo tunaamini litatusaidia," alisema Waziri Ndaki. Aliwataka wadau wengine wa ufugaji kushirikiana na serikali kupata mbegu bora za mifugo ili kuboresha hali ya ufugaji nchini na kuifanya sekta hiyo kuwa miongoni mwa zinazoliingizia taifa fedha nyingi bila kuzaa migogoro.

Akikabidhi dume hilo, Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbogo Ranches, Pirmohamed Mulla, alisema waliamua kutoa dume hilo kwa lengo la kuisaidia serikali kupata mbegu bora za mifugo.

Alisema dume walilolitoa lina uwezo wa kuzalisha mbegu 30,000 kwa mwaka endapo litaishi kwa miaka sita huku akieleza kuwa katika shamba lao dume hilo lingekuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu zisizozidi 150 katika kipindi cha uhai wake.

Alisema katika shamba lao uzalishaji wa mbegu wa dume hilo ni mdogo kutokana na kulitumia kwa njia ya asili ya kupanda lakini serikalini litatumika kwa njia ya kisasa ya uhawilishaji ambayo alisema ina tija zaidi.

Alisema dume hilo limekaguliwa na wataalamu na limeonekana kuwa na ubora wa hali ya juu na hivyo akaihakikishia serikali kwamba kama litatumika vizuri kuna uwezekano wa kuzalisha mbegu nyingi zaidi.

"Hili dume lina umri wa miaka mitatu na ndio umri sahihi wa kuanza kuzalisha, serikali ina wataalamu ambao watakaokamua mbegu za hili dume na kuzalishia mifugo mingine ambayo tuna uhakika wafugaji wakiitumia watafaidika zaidi," alisema Mulla.

Aliwataka wafugaji ambao wanahitaji mbegu za ng'ombe hao wanaweza kuzipata kwenye ranchi mbalimbali zilizoko nchini na kwamba hata serikalini zinapatikana.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa PanAfrican Energy Tanzania, Andy Hanna, alipotembelea banda la kampuni hiyo, wakati wa ufunguzi wa kongamano la nishati Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TCRA yasema sensa itasaidia kuboresha huduma za mawasiliano

**Martha Sambo,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imesema Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu ni muhimu kwa kila Mtanzania kwa kuwa itasaidia kuboresha huduma za mawasiliano.

Akizungumza na Nipashe jana kwenye viwanja vya maonyesho ya wakulima (Nanenane) vya John Mwakangale jijini Mbeya, Meneja wa TCRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John, alisema sensa ya watu na makazi itawezesha mamlaka hiyo kuboresha mawasiliano katika jamii kulingana na uhitaji wake.

Meneja alisema mamlaka hiyo inatamani kuona asilimia 80 ya watumiaji simu za mkononi wanafikiwa na mtandao kwa urahisi.

"Ukihesabiwa utatuwezesha kukuletea huduma bora za mawasiliano, sensa ni nafasi muhimu kwa watumiaji wa mawasiliano,niwaombe wananchi jitokeze kuhesabiwa," alisema Asajile.

Asajile alisema mamlaka hiyo haifikishi lengo lake la utoaji huduma kutokana na kukosa idadi maalumu ya watumiaji wa mawasiliano na kupitia sensa ya watu na makazi itarahisisha huduma za mawasiliano kuwafikia wananchi kwa urahisi.

Akizungumzia wizi kwa njia ya mtandao meneja huyo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini alisema mamlaka hiyo imeendelea kudhibiti kwa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaobainika kujihusisha na wizi huo.

"Kwa wale wote wanaojihusisha na wizi mtandaoni tunaendelea kuwashughulikia ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani, niwasisitize wananchi tuepuke kufanya utapeli hata kwa njia ya mtandao hatutavifumbia macho vitendo hivyo niwaombe sana tumieni vizuri mitandao ya kijamii na mitandao ya simu badala ya kufanya wizi."

Alisisitiza ni vyema wananchi wakashirikiana na mamlaka husika ikiwa ni pamoja na TCRA na Jeshi la Polisi kudhibiti vitendo hivyo vya uhalifu mtandaoni.

Mhandisi huyo wa TCRA alisema matumizi bora ya mitandao yana faida kubwa hususani kwenye sekta ya kilimo ikiwa wakulima watatumia vizuri.

Alisema wanatamani kuona asilimia 80 ya watumiaji wa simu za mkononi wanafikiwa na huduma za mitandao.

## TARI yabaini aina 50 miti ya matunda pori

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kupitia kituo chake cha Tumbi kilichoko mkoani Tabora kimefanya utafiti na kubaini kuwapo kwa zaidi ya aina 50 ya miti ya matunda pori kwenye misitu ya Miombo nchini yenye uwezo wa kuchangia usalama wa chakula endapo ikolojia yake itaendelezwa.

Akizungumza na gazeti hili katika mahojiano maalumu kwenye maonesho ya wakulima na wafugaji yanayofanyika kitaifa mkoani Mbeya, Mkurugenzi wa Kituo hicho cha TARI – Tumbi, Dk. Emanuel Mrema, alisema miti hiyo ya matunda pori pia imebainika kuwa na uwezo wa kutoa lishe na tiba ya kumaliza tatizo la udumavu.

Dk. Mrema alisema katika utafiti huo pia miti hiyo ya matunda pori inaweza pia utunzaji wa mazingira na kuongeza kipato kwa mkulima kwakuwa inauwezo mkubwa wa kuhimili hali ya ukame kwa kipindi kirefu ukilinganisha na miti mingine ya asili.

Mkurugenzi huyo wa TARI- Tumbi alitaja baadhi ya miti hiyo kuwa ni Ntonga ambayo inauwezo wa kusaidia kumaliza tatizo la udumavu na magonjwa yanayotokana na upungufu wa vitamini na viini muhimu kwa ajili ya tiba ya magonjwa ya binadamu na mifugo.

"Hii miti ya matunda pori inaweza kuwa chanzo muhimu sana cha chakula, lishe na dawa na kusaidia kupiga vita utapiamlo na upungufu wa vitamin A na C, amino asidi muhimu na madini kama chuma na zinki," alisema Dk. Mrema.

Mti mwingine wa matundapori ni Nizlchi ambao unasaidia kuongeza kiwango cha damu na kutibu magonjwa ya kifua huku mti wa Fulu ukisaidia kumaliza magonjwa ya tumbo.

Dk. Mrema alisema faida nyingine, ikisindikwa inaweza kutengenezwa juisi pamoja na mvinyo na mkulima kujiongezea kipato na kuondokana na hali ya umaskini.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema mkakati ulioko hivi sasa ni kuhakikisha wanaendeleza na uzalishaji wa miche ya miti ya asili na matunda ili miti hiyo muhimu isiweze kupotea kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa tayari ameshaagiza kituo hicho cha Tumbi kipande miti ya asili kwaajili ya kuhifadhi mazingira pamoja na kuwa chanzo muhimu cha lishe na dawa za magonjwa ya binadamu.

Kwa upande wake Mtafiti wa Kilimo misitu kutoka TARI- Tumbi, Kassim Masibuka, alisema tatizo kubwa lililokuwapo ni kukatwa kwa miti hiyo ambayo ipo katika tishio la kutoweka.

Alisema mkakati uliokuwapo hivi sasa ni kuendelea kuzalisha miti hiyo ya asili ya matunda na dawa kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi kutokana na kutumika pia kwenye kusaidia kilimo.

"Hii miti ya matunda pori katika nchi nyingine ndio inatumika kama dawa, kutengeneza juisi pamoja na mvinyo hivyo ni muhimu ikolojia yake ikatunzwa kwa gharama yoyote kwa manufaa ya nchi," alisema Masibuka.



# Zanzibar kushirikiana na Marekani kujenga uchumi, demokrasia, amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali iko tayari kushirikiana na Marekani katika masuala ya kiuchumi na ujenzi wa demokrasia na amani.

Othman aliyasema hayo ofisini kwake, Migombani mjini Zanzibar, alipozungumza na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, aliyetaka kufahamu utekelezaji wa masuala ya ushirikiano ukiwamo ujenzi wa demokrasia na utekelezaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar.

Alisema Zanzibar inaendelea kutekeleza na kutegemea sera ya uchumi wa huduma za utalii na ukarimu na kwamba suala la utulivu na amani ya kweli katika nchi linabaki kuwa na umuhimu wa pekee katika ujenzi na maendeleo ya nchi.

Uchumi huo pia, alisema unategemea kuwapo uwekezaji mkubwa wa aina na sekta mbalimbali na hakuna mwekezaji anayeweza kuwekeza katika taifa lisilokuwa na amani ya kweli.

Alisema viongozi kupitia SUK wanaendelea na juhudi ya kuondoa mgawanyiko na kuwaunganisha wananchi kuwa kitu kimoja jambo ambalo litasaidia katika kukuza uchumi na kuharakisha maendeleo.

Kuhusu SUK, Othman alisema suala hilo kuwamo katika katiba ni fursa muhimu ya kuisaidia nchi na viongozi kuandaa na kuweka mfumo bora na miundo imara ya kuimarisha serikali hiyo.

Alisema tayari kuna hatua na maendeleo makubwa ya uimarishaji wa suala hilo licha ya kwamba utekelezaji wake kwa baadhi ya masuala unakwenda polepole.

Kwa mujibu wa Othman, hali hiyo imeleta matumaini kwa wananchi na kuona kwa kuna jitihada kubwa zinazofanywa na viongozi wao ndiyo maana Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameshauri baraza la vyama vya siasa kuunda kikosi kazi kitakachopewa jukumu la kushughulikia masuala maalumu yanayohusu Zanzibar.

Naye Balozi Wright alisema Marekani itaendelea kushirikiana na Zanzibar katika masuala mbalimbali ikiwamo kuwakuza vijana wa Zanzibar kufaidi fursa za maendeleo na kiuchumi kupitia kilimo, ujasiriamali na kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza uchumi wa buluu Zanzibar kwa maendeleo ya wananchi.

Balozi huyo pia alisema hatua hiyo inatokana na serikali ya Marekani kuvutiwa na utekelezaji wenye matumaini wa SUK jambo ambalo litakuza demokrasia na kuimarisha amani nchini.

Alisema Marekani itaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika juhudi zozote za kuleta mageuzi ya kiuchumi na kisiasa yatakayohitajika katika sekta tofauti ikiwamo kuwaleta pamoja wawekezaji na wafanyabiashara wa Marekani na jumuiya za kimataifa kupitia makongamano kutoa fursa muhimu ya kuchangia juhudi za kuleta maendeleo Zanzibar.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), akizungumza na Balozi wa Marekani hapa nchini, Donald Wright, alipofika ofisini kwake, Migombani, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Sababu kupotea umeme zabainika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASILIMIA 17 ya umeme unapotea Zanzibar kutokana na baadhi ya watu kuunga umeme kinyume cha sheria.

Waziri wa Nishati na Madini wa Zanzibar, Shaibu Kaduwara, amesema wanaotumia umeme kinyume cha sheria ni kosa la jinai na atakayebainika atashtakiwa kwa kosa la kuhujumu uchumi wa nchi.

Kaduwara aliyasema hayo jana aliposhiriki katika msako uliopewa jina la 'Kaduwara' ambao umelenga kuwatafuta wananchi wanaojiunganishia nishati ya umeme kinyemela.

Alisema imebainika wako wananchi wengi wanaotumia umeme kinyume cha sheria kwa kujiunganishia majumbani, kitendo ambacho huliingizia hasara Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO).

Wizara yake, alisema imeanzisha operesheni hiyo ambayo lengo lake ni kufanya msako wa kuwatafuta watu wanaojipatia huduma muhimu ikiwamo majisafi na salama kinyume cha sheria.

Aidha, alisema imebainika wako baadhi ya wananchi wanaotumia huduma ya maji safi na salama kinyume cha sheria, kuikosesha shirika mapato yake kwa ajili ya kuendesha huduma za kikazi.

"Nimezindua operesheni 'Kaduwara' ambayo lengo lake ni kupambana na watu wanaotumia huduma muhimu za maji na umeme kinyume cha sheria ambao tunaweza kuwaita wahujumu uchumi," alisema.

Waziri huyo aliutaka uongozi wa ZECO kuhakikisha unakamilisha taratibu zote za kuwaunganishia wananchi umeme ambao wamekamilisha maombi yao.

Alisema lengo la serikali ni kuwapatia wananchi huduma za majisafi na umeme kwa ajili ya kurahisisha na kuyafikia maendeleo ya wananchi wakiwamo wa vijijini.

Naye fundi wa ZECO, Juma Mussa, alisema wamebaini wako watu wanaotumia huduma ya umeme kwa kuunganisha umeme kinyume cha sheria.

Alisema matumizi ya aina hiyo hayakubaliki kwa kuwa husababisha hasara kubwa katika matukio ya maafa ya nyumba kupata hitilafu za umeme.

## SMZ yasisitiza kutambua huduma za taasisi za bima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kutambua mchango wa mashirika ya bima katika kukuza uchumi wa nchi na kusaidia wananchi wanapokutwa na majanga.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo jana alipokutana na uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Bima Tanzania (TIRA) na kukabidhi miongozo ya kiutendaji afisini kwake, Vuga, Zanzibar.

Alisema serikali inaridhishwa na mienendo ya mashirika hayo katika kusaidia jamii hasa wanapokutwa na majanga hatua ambayo inasaidia kupunguza athari zinazojitokeza wanapokumbwa na maafa.Hemed alifurahishwa na uwapo wa mpangowautekelezajiwamamlaka hiyo na kuwahakikishia kuwa serikali ya Zanzibar itasimamia utekelezaji kwa vitendo.

Pia alisema mbali na uwapo wa sheria mbalimbali nchini, bado wadau wa bima wana haki ya kuishauri serikali kurekebisha sheria ili kuendana na hali zao za kiutendaji kwa lengo la kuboresha huduma zao ziwafae zaidi wananchi.

Alisema bado jamii inahitaji elimu ya ziada kuhusiana na umuhimu wa kukata bima hivyo, ameutaka uongozi huo kuongeza juhudi za kuwafikia wananchi hasa wawekezaji, wafanyabiashara na makundi mbalimbali ili kujiunga na huduma hizo.

Naye Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Abdallah Saqwere, alisema mpango waliomkabidhi umejumuisha suala la ajira, mfumo wa usambazaji bima kidigitali na bima ya takaful.

Alisema TIRA imeshawakaribisha wawekezaji katika takaful pamoja na kueleza azma yao ya kuhamasisha ukataji wa bima katika maeneo ya kijamii ikiwamo masoko, bidhaa zinazoingia nchini na maeneo mengine mbalimbali.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

KATIKA MAHAKAMA YA TANZANIA

MASJALA NDOGO YA TEMEKE

(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)

MIRATHI NA 50 YA MWAKA 2022.

MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU JOHN MUGONA

RAHELI JOHN MUGONA.........................MWOMBAJI

**TAARIFA YA KAWAIDA**
(kanuni ya 75)

Watu wote wanodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 11 mwezi w Julai, 2022.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 16 mwezi wa Mei, 2022

HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAJOGI (T) CO. LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 145 AMA** aina ya **SUZUKI**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/278616/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GAPOIL TANZANIA LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 207 ACQ – STATION WAGON.** Chassis namba **069374.** Engine namba **403006.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/298092/2022.**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA
CIVIL 13/2020
HEKI BUSINESS CO.LTD............... APPLICANT
VERSUS
TANZATHAI IR CO.LTD.......... RESPONDENT
TO:- TANZATHAI
NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing/mention on **15 day of 8, 2022 at 9:00 am.**
Before Hon **A . E . KATEMANA RM/SRM**
**YOUR ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail and you may bring with you all required documents in support of your case.
**Given under my hand and the seal of the court this 3 day of 8,2022**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA VYETI



**THEODAT ELIGIUS MYALLA** ANATANGAZA kupotelewa na **CHETI CHA FORM FOUR(CSEE)** chenye Index Number: **S 1529-0037** Kilichotolewa na Baraza la Mtihani la Taifa kupitia shule ya **CENTENARY SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013** na pia **CHETI CHA FORM SIX(ACSEE)** Index Number: **S0685-0602** Kilichotolewa na Baraza la Mtihani Taifa kupitia shule ya **NAMABENGO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi **RB** namba **SO/RB/1012/2017**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**EZEKIEL ELISANTE GEREYAN** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T504DFD** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **ARU/ARU/RB/305796/2022**

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**ELISANTE GEREYAN** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 482BZM** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **ARU/ARU/RB/298815/2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
Kumb. Na. MMC/LD/7617/21
Tarehe: 01/08/2022
SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999
KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI
BARUA YA TOLEO YENYE KUMBUKUMBU NA: Y/280/10/PMM
MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: SHABAN KHALFANI MHANDO
ARTHI: KIWANJA NA. 280 KITALU 'Y' VIBANDANI
MUOMBAJI: SAID IDD KINYOGOLI

Taarifa inatolea kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana,irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA- MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO.**

Valency H.K
KNY; MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO
MKOA WA MOROGORO

KATIKA SHAURI LA MADAI NAMBA 33/2022

DHIDI YA

ENOCK PETER.............................................MDAI

DHIDI YA

EMMANUEL REMMY MAHWISA..................MDAIWA

**WITO WA KUITWA SHAURINI**
EMMANUEL REMMY MAHWISA

Popote ulipo unatakiwa ufike katika mahakama ya wilaya ya morogoro tarehe 30/08/2022 ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 02 mwezi wa 08 mwaka 2022

R.R. KASELE
PRINCIPAL RSIDENT MAGISTATE
MOROGORO.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMOS RASUL KILONZO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS STAR** yenye namba za usajili **MC 222 CDX,** chasis namba **MD625AF74JIN00266,** engine namba **AF7NJI200203,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/OST/RB/245992/2022**


OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

KWA HABARI MOTOMOTO
USIKOSE GAZETI
LAKO LA NIPASHE KILA SIKU



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wajackoya akana kumuunga mkono Odinga

**NAIROBI,** KENYA

MGOMBEA wa urais wa chama cha Roots George Wajackoya amekana madai kwamba amemuidhinisha mgombea wa muungano wa Azimio la Umoja Raila Odinga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Wajackoya alidai kwamba video inayosambazwa mitandaoni ikimuonyesha akimuidhinisha Odinga imebadilishwa ili kuwapotosha wafuasi wake.

"Sijamuidhinisha Odinga, bado nipo katika kinyang'anyiro cha kuchukua uongozi wa Kenya," alisema Wajackoya.

Aidha, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na mipaka nchini Kenya, Wafula Chebukati, alisema tume hiyo ipo tayari kuandaa uchaguzi mkuu na inaamini kuwa utakuwa wa haki, uwazi, unaoaminika na unaoweza kuthibitishwa na kuwataka raia wa Kenya kuwa na imani na tume hiyo.

**SHULE ZAFUNGWA KUPISHA UCHAGUZI**

Katika hatua nyingine wadau wa elimu nchini Kenya walishutumu agizo la serikali la kuamrisha kufungwa kwa shule zote nchini humo ikiwa ni wiki tatu tangu kufunguliwa.

Wadau wa elimu nchini Kenya walieleza kuwa hatua ya serikali kuamuru kufungwa kwa shule hizo wakati tarehe ya uchaguzi ilikuwa inafahamika na wizara ya elimu, waliitaja kama ni ya kushtukiza na isiyofaa.

**MZIGO KWA WAZAZI**

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na VOA ilieleza kuwa wazazi wanalazimika kuweka mipango ya kusafirisha watoto wao wanaosoma kwenye shule za malazi badala ya kupanga kuwaondoa shuleni kwa mapumziko ya katikati ya muhula mwishoni mwa wiki hii kama ilivyoainishwa kwenye kalenda ya masomo iliyotolewa na wizara ya elimu.

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa jukumu lingine linalowakabili wazazi ni kuwawezesha watoto wao kurejea shuleni Alhamisi wiki ijayo siku mbili baada ya kukamilika kwa upigaji kura.

Inaelezwa kuwa serikali ya Kenya ilisema tangazo lake la ghafla ni la kuiwezesha tume ya uchaguzi IEBC kuwa na muda zaidi wa kujiandaa kwa uchaguzi wa Jumanne wiki ijayo, huku wadau wakieleza kuwa hapakuwapo na maelezo ya kina kabla ya tangazo hilo.

**KUVURUGWA KWA MAANDALIZI YA MITIHANI**

Inatajwa kuwa shule nyingi nchini humo zimekuwa zikitekeleza majaribio ya tathmini ya katikati ya muhula ambayo inatathmini wanafunzi wiki tatu baada ya kukamilika kwa mapumziko ya muhula uliopita.

Awali, Waziri wa Elimu, Profesa George Magoha alionyesha mafadhaiko yake kuwa huenda kalenda ya masomo ikavurugwa tena kutokana na uchaguzi mkuu.

Kwa mujibu wa kalenda ya masomo ya Kenya, muhula wa pili una wiki 10 za kujifunza na ulitarajiwa kukamilika Septemba 16 lakini iwapo uchaguzi utakumbwa na utata au hitilafu, huenda shule zikalazimika kufungwa zaidi.

Wadau wa elimu akiwemo mwenyekiti wa chama cha wazazi Kenya, Nicholas Maiyo alisema kwamba patahitajika kuwapo ushauri wa kina kuwezesha urejeleaji wa masomo kwa njia salama.

Pia wadau wanaeleza kuwa mkakati wa ufundishaji unaweza kuathirika zaidi na walimu huenda wasipate nafasi ya kuwatayarisha wanafunzi ipasavyo.

Ni siku sita tu pekee zimebakia kwa Kenya kufanya uchaguzi wake mkuu, wa saba baada ya miaka 30 chini ya mfumo wa vyama vingi, na wa 12 baada ya kujinyakulia uhuru miaka 59 iliyopita.

**VOA**

# Jeshi DRC laua waasi 11 wa ADF

**CONGO,** DRC

JESHI la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) limebainisha kuwa limewaua waasi 11 wa kundi la wanamgambo la Allied Democratic Forces (ADF) ambalo kundi la kigaidi la Islamic State linadai ni mshirika wake, mashariki mwa nchi hiyo.

ADF ni moja ya makundi yanayofanya ukatili mkubwa kati ya zaidi ya makundi 120 yaliyopo katika eneo la mashariki mwa DRC yenye mzozo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA kundi hilo limelaumiwa kwa maelfu ya vifo katika mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri kwa mashambulizi ya mabomu mwaka jana nchini Uganda.

Msemaji wa jeshi la Congo katika mji wa Beni katika jimbo la Kivu Kaskazini, Kepteni Antony Mualushayi, alisema wanajeshi waliwaua wapiganaji 11 wa ADF mwazoni mwa wiki hii.

"Siku moja kabla wanajeshi waliwaua wapiganaji wanane wa kundi la Mai Mai Mazembe katika wilaya ya Lubero huko Kivu Kaskazini katika mapigano yaliyokuwa yakiendelea," alisema Mualushayi.

Rais wa DRC, Felix Thisekedi alibadilisha viongozi wa kiraia wa Kivu Kaskazini na Ituri na kuwaweka maofisa wa kijeshi katika harakati za kumaliza ghasia, ikidaiwa kuwa pamoja na mabadiliko hayo mashambulizi ya waasi dhidi ya raia yaliendelea.

**VOA**



Mgombea wa kiti cha urais nchini Kenya, Prof. George Wajackoyah, akizungumza wakati wa kampeni. **PICHA: MTANDAO.**

# Marekani yaidhinisha vikwazo vipya dhidi ya kampuni Russia

**WASHINGTON,** MAREKANI

WASHINGTON imepiga kura juu ya vikwazo vipya dhidi ya kampuni za Russia na matajiri kutoka ukanda huo walioko karibu na Rais Vladimir Putin.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Washington vikwazo vipya vya kiuchumi dhidi ya Russia vimetangazwa, huku vikilenga hasa makampuni na matajiri walio karibu na Rais Vladimir Putin.

Miongoni mwa matajiri hao walitajwa kuwa ni Andrey Guryev, mwanzilishi wa kampuni ya mbolea Phosagro, mshirika wa karibu wa Putin na mjumbe wa zamani wa serikali ya Russia, ambaye mali zake zimezuiliwa na Ofisi ya Udhibiti wa Mali za Kigeni (OFAC), na inaelezwa kuwa anamiliki mali kubwa zaidi ya kibinafsi huko London, iliyoko nyuma ya Jumba la Buckingham.

Pia inaelezwa kuwa meli yake ambayo ilimgharimu dola milioni 120 na kununuliwa mwaka 2014 pia inalengwa na Washington, na kwa mujibu wa Wizara ya Fedha ya Marekani, meli hiyo imezima kifaa chake cha utambuzi wa eneo ilipo ili kuepusha kukamatwa.

Aidha, imeelezwa kuwa kampuni yake haijaathiriwa na vikwazo hivyo wala miamala inayohusiana na mbolea na bidhaa nyingine za kilimo havitalengwa na vikwazo hivyo.

Waziri wa Fedha wa Marekani, Janet Yellen alibainisha kuwa washirika wa Putin walitajirika na kufadhili maisha ya kifahari nchini humo.

Waziri huyo alisisitiza kwamba "kila chombo katika hazina kitatumika kuhakikisha kuwa vigogo na matajiri wa Russia na waungaji mkono wa Kremlin wanawajibishwa kwa kushiriki kwao katika vita ambavyo vimegharimu maisha ya watu wengi," alisema.

Pia ilibainishwa kuwa mtoto wa Andrey Guryev ambaye kwa upande wake, tayari amewekewa vikwazo na nchi kadhaa, analengwa pia na vikwazo vya Washington.

**RFI**

# MTIBWA SUGAR YAWEKA REKODI MPYA LIGI BARA

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, Mtibwa Sugar ambayo ilikuwa na matokeo yasiyoridhisha katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika hivi karibuni, imetangaza kuachana na wachezaji wake 20 walioitumikia timu hiyo, imeelezwa.

Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadhi Juma, aliliambia gazeti hili uamuzi wa kuwatema wachezaji hao umefanyika kwa ajili ya kupisha ujenzi wa kikosi kipya kinachotarajiwa kuwapa matokeo mazuri kwenye msimu mpya.

Juma alisema wanahitaji kuingia katika msimu mpya wakiwa imara na kujiondoa na mwendo wa kusuasua kama ilivyokuwa kwenye misimu miwili iliyopita.

Kocha huyo alisema, wameamua kufanya mabadiliko makubwa katika kikosi chao ili kulinda hadhi na heshima ya klabu hiyo.

"Tumepunguza wachezaji wengi, tumesajili baadhi ya wachezaji wengine wakiwa ni wazoefu katika ligi, vile vile tumepandisha nyota vijana waliotwaa ubingwa wa Ligi ya Vijana ya U-20 iliyomalizika hivi karibuni.

Tunaamini mabadiliko tuliyoyafanya yataenda kufanya kitu, tumeamua kuangalia upande mwingine kwa sababu tumefanya vibaya sana katika misimu miwili mitatu hivi, kwa hiyo tumefanya mabadiliko makubwa ili kuanza upya," alisema kocha huyo.


Aliongeza uamuzi wa kusajili wachezaji wazoefu ambao watashirikiana na nyota vijana unatarajiwa kutengeneza timu nzuri itakayorudisha heshima ya Mtibwa Sugar.

"Hakuna ugeni katika mpira, soka ni lile lile tu, kwa hiyo kwa upande wetu tunaamini tumetengeneza timu imara," Juma alisema.

Hiyo ni rekodi kwa timu ya Ligi Kuu Bara kuacha idadi kubwa ya wachezaji kiasi hicho kwa miaka ya hivi karibuni.

Misimu miwili iliyopita, Mtibwa Sugar imenusurika kushuka daraja dakika za mwisho kwa kuangukia kucheza mechi za mchujo 'play off' na hatimaye kubakia kwenye Ligi Kuu.

Tayari Mtibwa Sugar imetangaza kusajili Mohamed Makaka kutoka Ruvu Shooting, Charles Ilamfya (KMC FC), Idd Mobby (Geita Gold FC), na Mapinduzi Balama wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.




Mkazi wa jijini Mbeya, Ojilloh Mwaikimba akiwa ameshikilia zawadi ya mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 58.6 aliyoshinda baada ya kubashiri kwa usahihi matokeo ya mechi 12 za ligi mbalimbali duniani kupitia droo iliyoendeshwa na Kampuni ya M-BET nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinara wa pikipiki kupewa nyumba

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MSHINDI wa mashindano ya pikipiki yaliyoandaliwa na Taasisi ya Global Peace Advocacy For Conflict Resolution ngazi ya taifa yatakayofanyika Agosti 30, mwaka huu jijini hapo atapata zawadi ya nyumba, imefahamika.

Lengo la mashindano hayo yatakayojulikana kwa jina la Tanzania Royal Tour Rally 2022 ni kuunga mkono juhudi za Rais, Samia Suluhu Hassan, katika kutangaza fursa za utalii wa hapa nchini kupitia filamu ya Royal Tour.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Ryamoja Mafuru, alisema wameandaa mashindano hayo ili kuwawezesha waendesha pikipiki kubeba ujumbe wa kuhamasisha utalii nchini.

Mafuru alisema, mbio hizo katika ngazi ya wilaya zitaanza kufanyika Agosti 13, mwaka huu na awamu ya pili itakuwa ni Agosti 17, mwaka huu ambapo kutakuwa na zawadi kwa watakaofanya vizuri kwenye mashindano hayo.

"Tunawaomba wadau wa mchezo huu wajitokeze kushiriki katika mashindano haya, tumejipanga vizuri na tunatarajia kumkabidhi mshindi zawadi ya nyumba iliyopo Dodoma katika eneo la Iyumbu," alisema Mafuru.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya State Aviation, Amour Abdallah alisema kampuni hiyo itatoa helikopta kwa ajili ya kuhamasisha tukio hilo ili kuwawezesha vijana wakiwamo madereva ambao ni msaada muhimu katika kuchangia maendeleo ya taifa.

## Mwaikimba asimulia alivyoshinda M-BET

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Manchester City, Ojilloh Mwaikimba wa jijini Mbeya, ameshinda Sh. milioni 58. 6 baada ya kubashiri kwa usahihi matokeo ya mechi 12 za ligi mbalimbali duniani kupitia droo ya Kampuni ya M-BET Tanzania.

Mwaikimba alisema haikuwa rahisi kushinda fedha hizo kutokana na ugumu wa kubashiri mechi na hasa kipindi ambacho ligi zilikuwa zimesimama huku timu chache zikienda kufanya mazoezi ya kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

Alisema pamoja na changamoto hiyo, Mwaikimba ambaye ni mwalimu kitaaluma, aliweza kufanya ubashiri wake kwa umakini mkubwa na kufanikiwa kupata fedha hizo.

Alifafanua kuwa alishinda fedha hizo wiki kadhaa zilizopita, lakini kutokana na tatizo la usajili wa simu yake hakuweza kupata fedha hizo katika muda huo kutokana na utaratibu wa kampuni ya M-BET.

Mkurugenzi wa Masoko wa M-BET Tanzania, Allen Mushi, alisema wataendelea kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria na taratibu na kuwaomba watu wenye usajili tofauti na kitambulisho cha Taifa kufanya marekebisho.

"Nampongeza Mwaikimba kwa ushindi huu mnono ambao utamwezesha kuwa miongoni mwa washindi wetu ndani ya nyumba ya mabingwa, Pia nawakumbusha wananchi kushiriki katika zoezi la Sensa la Taifa," alisema Mushi.

## Simba SC Bahi yatoa msaada

**Na Peter Mkwavila, BAHI**

MASHABIKI wa Simba wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma wametoa misaada mbalimbali katika Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya cha Bahi ikiwa ni sehemu ya kuelekea Tamasha la Simba Day litakalofanyika Agosti 8, mwaka huu.

Vitu vilivyotolewa msaada vina thamani ya Sh. 500,000 lakini pia wanachama hao wamechangia damu katika hospitali hiyo.

Akizungumza wakati wanakabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Simba wa Tawi la Bahi, Samwel Galulet alisema lengo la kutoa misaada hiyo ni kuwajali wagonjwa kwa vitendo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, aliwapongeza mashabiki wa Simba kwa kutumia sherehe za Simba Day kuwakumbuka wagonjwa ambao wanahitaji faraja.

Munkunda pia amewataka mashabiki hao kuhamasishana kushiriki Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TRAORE AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikamgeukia winga wa Wolves, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, ikiwa hawataweza kufikia makubaliano na AS Roma kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye miaka 23. ***(90min)***

### FODEN MAMBO SAFI

KIUNGO wa kati wa Timu ya England, Phil Foden mwenye umri wa miaka 22 amekubali mkataba mpya wa muda mrefu ambao utamfanya alipwe pauni 225,000 kwa wiki katika klabu ya Manchester City. ***(Mail)***

### UNITED, CHELSEA VITANI

KLABU ya Manchester United na Chelsea zinamfuatilia mshambuliaji wa Leicester City, Jamie Vardy mwenye umri wa miaka 35, ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa. ***(90min)***

### DAMSGAARD KIMEELEWEKA

DAU la Brentford la pauni milioni 16.7 kumnunua kiungo wa kati wa Denmark, Mikkel Damsgaard mwenye umri wa miaka 22 limekubaliwa na Sampdoria. ***(Sky Sports)***

### WAARABU NA RONALDO

KLABU moja ya nchini Saudi Arabia imesema ofa yao ya kumnunua mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, itabakia mezani baada ya Kombe la Dunia iwapo mustakabali wa mchezaji huyo hautasuluhishwa. ***(CBS Sports)***

### GOMEZ ANUKIA CITY

KLABU ya Manchester City imeanza mazungumzo na Anderlecht kuhusu beki wa kushoto wa Hispania, Sergio Gomez. Mchezaji huyo mwenye umri wa chini ya miaka 21 anatajwa kama mbadala wa nyota wa Brighton, Marc Cucurella (24). ***(Times)***

### ANGELINO KUMRITHI CUCURELLA

KLABU ya Brighton inamfikiria beki wa pembeni wa RB Leipzig, Angelino kuchukua nafasi ya Marc Cucurella, ambaye amewavutia Chelsea. ***(Sky Sports Germany, via Mail)***

### LEICESTER YAIGOMEA NEWCASTLE

KLABU ya Leicester City imekataa ofa ya pili yenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 40, kutoka kwa Newcastle United kwa ajili ya kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, James Maddison mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports)***

### FOFANA AIOTA CHELSEA


MLINZI wa Leicester City, Wesley Fofana amedokeza kuhusu hatua yake ya kuondoka uwanja wa King Power kwa kuiondoa akaunti ya Leicester City kwenye mtandao wake wa kijamii. Chelsea wameonyesha nia ya kumnunua Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 21 msimu huu wa joto. ***(Leicester Mercury)***

### FULHAM YAMTAKA BAILLY

KLABU ya Fulham imewasilisha ofa ya kumnunua mlinzi wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### WALKER-PETERS SOKONI

CHELSEA wana nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Southampton na Timu ya Taifa ya England, Kyle Walker-Peters mwenye umri wa miaka 25. ***(Guardian)***



# POGBA AKATAA KUPASULIWA GOTI

## Lakini imethibitika atakuwa nje kwa muda wa wiki tano kabla ya...

**LYON, Ufaransa**

PAUL Pogba ameripotiwa kuchagua kutofanyiwa upasuaji baada ya kukutana na daktari mtaalamu wa kuchunguza jeraha lake la goti na huenda hata akarejea kucheza ndani ya wiki tano pekee.

Baada ya kuondoka Manchester United na kurejea Turin, Pogba alikuwa na matumaini ya kuanza upya, lakini aliumia goti wiki za mwanzo za kipindi chake cha pili akiwa na Juventus.

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa alilalamikia jeraha lake wakati akiwa na Juve katika ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani na uchunguzi wa awali uliifanya klabu hiyo ya Italia kutangaza alikuwa na jeraha la goti.

Kulikuwa na hofu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 anaweza kukosa mwaka mzima wa msimu huu ikiwa angechagua kufanyiwa upasuaji.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport, Pogba alishauriana na daktari maarufu duniani wa upasuaji wa goti Profesa, Bertrand Sonnery-Cottet mjini hapa na ikakubaliwa angefanyiwa matibabu baada ya upasuaji, ikimaanisha anapaswa kurejea uwanjani takribani wiki tano.

Pogba alikuwa sehemu muhimu ya Timu ya Ufaransa iliyonyanyua Kombe la Dunia mwaka 2018, na habari hii itaongeza nafasi yake ya kuwa fiti kutetea taji hilo nchini Qatar baadaye mwaka huu.

Pogba alikaa Juve kwa miaka minne kati ya 2012 na 2016, akishinda mataji manne ya Serie A katika kipindi hicho kabla ya kuhamia United kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia ya pauni milioni 89.3.

Michuano ya Kombe la Dunia itaanza Novemba 21 nchini Qatar, na Kocha Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps angetaka Pogba ambaye amaichezea mechi 91 timu hiyo awe amethibitisha yuko fiti kabla ya michuano hiyo kuanza.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,019,3

MECHI KALI
FENERBAHCE
VERSUS
SLOVACKO
1 | 1.38
X | 4.64
2 | 7.66

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HENDERSON : UNITED HAWAKUNITENDEA HAKI



**LONDON, England**

DEAN Henderson amekiri alikuwa 'akikasirishwa' na Manchester United baada ya kupoteza namba katika msimu wa 2021/22 ndani ya timu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye hivi majuzi alijiunga na Nottingham Forest kwa mkopo kutoka kwa Mashetani Wekundu hao, pia alikiri alikataa ofa nyingi za mkopo msimu uliopita baada ya kuahidiwa atakuwa chaguo la kwanza pale United.

Akizungumza na TalkSport, Henderson alisema: "Kusema kweli, imekuwa miezi 12 migumu zaidi katika maisha yangu ya soka. Imekuwa ngumu na nina furaha sana ninaingia upande mwingine.

"Mazungumzo niliyofanya na United baada ya Euro nilikuwa narudi Old Trafford kuwa namba moja. Nilipata COVID na niliporudi nilipaswa kuwa namba moja.

"Lakini hakuna aliyefuata walichoniambia. Ilisikitisha pia kwa sababu nilikataa mikopo mingi mizuri msimu uliopita wa joto.

"Ni uhalifu katika umri wangu, nilipoteza miezi 12. Nilikuwa na hasira. Nilifanya kazi kwa bidii nje ya uwanja ili kujiweka bora siku baada ya siku. Sasa natazamia msimu mzuri na Forest."

Alipoulizwa kuhusu kocha mpya Erik ten Hag, na kama walizungumza chochote kabla ya kuhamia Forest, Henderson alijibu: "Sikuzungumza naye, sikutaka hata kumwona kwenye mazoezi kwa sababu. Nilijua pengine angetaka kunibakiza.

# Klopp afurahia Jota kubakia

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp alifurahishwa na kuthibitishwa kwa mkataba mpya wa muda mrefu wa Diogo Jota na Liverpool, ambapo fowadi huyo sasa atacheza hapo kwa miaka mingi.

Liverpool ilitangaza kuongezwa mkataba kwa Jota jana huku mkataba huo mpya ukiripotiwa kumalizika mwaka 2027.

Baada ya Mohamed Salah vile vile kukubaliana masharti mapya na Darwin Nunez kununuliwa kutoka Benfica, Liverpool inaingia katika msimu mpya wa Ligi Kuu England ikiwa na safu kali ya ushambuliaji licha ya kuondoka kwa Sadio Mane.

Akiwa na wastani wa kufunga bao kila baada ya dakika 157 katika mashindano yote, Jota alimzidi uwezo Mane (dakika 192) katika kipindi hiki, huku kiwango chake cha asilimia 17.7 cha kupiga shuti kuwa ubora zaidi kwa asilimia 17.5.

Hata hivyo, hizi sio sifa pekee za thamani kwa Klopp, ambaye aliiambia tovuti rasmi ya Liverpool: "Ni habari nzuri na nzuri, naweza kusema.

"Sifa zake ziko wazi. Anafunga mabao - sio ubora mbaya - anafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya timu, uchezaji wake wa kushinikiza uko kwenye kiwango cha kushangaza, anaweza kucheza katika safu zetu zote za ushambuliaji, na ana uwezo wa ajabu."



HABARI MICHEZO

301,493/-

# SERENGETI YAWAPA ZAWADI YA UBINGWA SIMBA QUEENS

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI Mkuu wa Ligi ya Soka ya Wanawake Nchini, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Serengeti Lite, imekabidhi zawadi ya hundi yenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa mabingwa wa ligi hiyo, Simba Queens.

SBL imetoa hundi hiyo siku chache baada ya ligi hiyo msimu wa 2021/2022 kumalizika, ambapo Simba Queens waliibuka washindi kwa kuwafunga Mlandizi Queens mabao 2-1 na kutetea ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

Ligi ya wanawake imekuwa ikiongezeka mvuto na ushindani tangu SBL kupitia bia yake ya Serengeti Lite kuingia kama mdhamini mkuu.

Mkurugenzi wa Sheria wa SBL, Lucia Minde alisema udhamini huo umesaidia kuibua vipaji vya wanawake katika soka na pia timu zenye ushindani mkali ambazo zimeweza kuitambulisha vyema ligi hiyo.


"Tunayofuraha kuona vipaji vipya vya soka kwa wanawake vinaendelea kujitokeza kutokana na udhamini wetu ambao umesaidia kuweka mazingira mazuri na wezeshi kwa wanawake kucheza mpira," alisema Lucia.

Aliongeza Serengeti Lite inajivunia kuwa mdhamini wa ligi hiyo na kuongeza udhamini huo umeongeza ushiriki wa wanawake katika michezo na hususani mpira wa miguu.

"Mpira wa miguu siyo tu burudani, ni shughuli ya kiuchumi ambayo imeajiri watu wengi duniani. Wanawake wanaoshiriki katika mchezo huu maarufu na wenye mashabiki wengi duniani wanajipatia kipato kwa ajili ya kuendesha maisha yao," alisema ofisa huyo.

Kwa mujibu wa TFF, miaka ya nyuma ilikuwa ni vigumu kwa timu kwenda kucheza mechi za ugenini kutokana na ukata. Ilikuwa ni vigumu kwa timu kumudu gharama za usafiri, malazi na nyinginezo kwa ajili ya kucheza mechi za ugenini lakini kwa sasa baada ya udhamini wa Serengeti Lite hilo sio tatizo kubwa tena.

Udhamini wa Bia ya Serengeti Lite kwa ligi ya wanawake ni mwendelezo wa ufadhili kwa michezo unaofanywa na SBL kupitia bidhaa zake mbalimbali ikiwamo bia ya Serengeti Premium Lager ambayo ni mdhamini mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars).




# KMKM yaota makundi CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wamesema malengo yao makubwa msimu huu ni kuhakikisha wanafika hatua ya makundi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu alisema timu yake inaendelea vyema na maandalizi kuelekea mashindano hayo ya kimataifa pamoja na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar.

Msimu alisema wanajipanga na kuwaimarisha wachezaji wao ili wafanye vizuri katika michuano hiyo na kusisitiza wamechoka kuondolewa mapema.

Aliongeza ili kufanikisha hilo, timu hiyo ilianza mazoezi mapema na wachezaji wote ambao wanaunda kikosi cha KMKM wamewasili kambini.

"Wachezaji wote wa KMKM ambao mwalimu anampango nao katika msimu huu tayari wamewasili na kuanza mazoezi, KMKM tunauzoefu mkubwa katika michuano hii lakini kwa msimu huu hatutaki tuwe wazoefu wa kushiriki tu, tunataka tukafanye vizuri," alisema kocha huyo.

Aliongeza ndani ya wiki hii watatangaza kikosi chao kamili walichokisajili ambacho kinaundwa na wachezaji wapya waliletwa ili kuziba mapengo ya nyota waliondoka na wale watakaoachwa.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/22 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.29 | 3.29 | 3.09 |
| 02. 06/08/22 | 17:00 | Bristol City vs Sunderland | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 03. 06/08/22 | 17:00 | QPR vs Middlesbrough | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 04. 06/08/22 | 17:00 | Reading vs Cardiff | 2.44 | 3.18 | 2.94 |
| 05. 06/08/22 | 17:00 | Swansea vs Blackburn | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 06. 06/08/22 | 17:00 | Burton vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.33 | 2.88 |
| 07. 06/08/22 | 17:00 | Charlton vs Derby | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 08. 06/08/22 | 17:00 | Exeter vs Port Vale | 2.53 | 3.17 | 2.82 |
| 09. 06/08/22 | 17:00 | Fleetwood Town vs Plymouth | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 10. 06/08/22 | 17:00 | MK Dons vs Sheffield Wed | 2.61 | 3.21 | 2.71 |
| 11. 06/08/22 | 17:00 | Shrewsbury vs Accrington | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 12. 06/08/22 | 17:00 | Barrow vs Bradford City | 2.59 | 3.13 | 2.78 |
| 13. 06/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 14. 06/08/22 | 17:00 | Hartlepool vs AFC Wimbledon | 2.89 | 3.24 | 2.44 |
| 15. 06/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 16. 06/08/22 | 18:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 17. 06/08/22 | 21:30 | Hansa vs Arminia Bielefeld | 2.64 | 3.34 | 2.59 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 04 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2890 | Qingdao Red Lions vs Yanbian Longding | 7.45 | 4.22 | 1.37 |
| 17:00 | 4513 | FK Liepaja vs BFC Daugavpils | 1.30 | 4.91 | 8.05 |
| 18:00 | 2928 | AL Salt vs FC Maan | 1.75 | 3.30 | 4.43 |
| 18:30 | 4432 | AEK Larnaca vs Partizan | 2.93 | 3.23 | 2.38 |
| 19:00 | 1066 | PK-35 vs TPS Turku | 3.48 | 3.48 | 1.90 |
| 19:00 | 1462 | Skeid Fotball vs Ranheim | 3.24 | 3.58 | 1.95 |
| 19:00 | 2217 | Mjondalen vs Raufoss | 2.15 | 3.45 | 2.91 |
| 19:00 | 2270 | Sandnes Ulf vs Sogndal | 2.11 | 3.55 | 2.91 |
| 19:00 | 2613 | Tampere United vs FC Honka/Akatemia | 2.56 | 3.78 | 2.25 |
| 19:00 | 3005 | KuPS Kuopio vs BSC Young Boys | 6.48 | 4.35 | 1.46 |
| 19:00 | 3607 | Rigas Futbola Skola vs Hibernians | 1.63 | 3.93 | 4.94 |
| 19:00 | 3619 | Fredrikstad vs Stabaek | 3.29 | 3.53 | 1.95 |
| 19:00 | 3783 | FC Jazz vs Musa Pori | 2.13 | 3.83 | 2.70 |
| 19:00 | 4810 | Kfum Oslo vs Aasane Fotball | 1.50 | 4.22 | 5.10 |
| 19:00 | 5922 | Brann vs IK Start | 1.21 | 5.88 | 9.40 |
| 19:30 | 1343 | Smouha Club vs Ceramica Cleopatra | 2.49 | 3.16 | 2.81 |
| 19:30 | 1408 | Eastern Company SC vs Enppi Club | 3.21 | 3.06 | 2.29 |
| 20:00 | 1544 | Shakhter Soligorsk vs CFR Cluj | 3.89 | 3.43 | 1.92 |
| 20:00 | 2097 | Fenerbahce vs Slovacko | 1.38 | 4.64 | 7.66 |
| 20:00 | 2496 | CSKA Sofia vs St Patricks | 1.54 | 3.98 | 5.85 |
| 20:00 | 2529 | Maccabi Tel Aviv vs Aris Salonica | 2.36 | 3.23 | 2.97 |
| 20:00 | 2637 | Lillestrom vs Royal Antwerp | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 20:00 | 2896 | AIK Football vs Shkendija | 1.43 | 4.51 | 6.62 |
| 20:00 | 3309 | Molde vs Kisvarda FC | 1.42 | 4.44 | 7.06 |
| 20:00 | 3727 | Osters IF vs Utsiktens BK | 1.79 | 3.72 | 4.28 |
| 20:00 | 3915 | Jonkopings Sodra vs Vasteras SK | 2.79 | 3.45 | 2.43 |
| 20:00 | 4941 | Neftchi Baku vs Rapid Vienna | 3.38 | 3.33 | 2.11 |
| 20:00 | 5204 | Slavia Prague vs Panathinaikos | 1.81 | 3.60 | 4.15 |
| 20:00 | 5898 | Malmo vs Dudelange | 1.25 | 5.63 | 11.06 |
| 20:00 | 5913 | Orgryte IS vs AFC Eskilstuna | 2.12 | 3.77 | 3.10 |
| 20:30 | 1272 | Zorya Lugansk vs Universitatea Craiova | 2.92 | 3.22 | 2.40 |
| 20:30 | 3906 | Hamrun Spartans vs Levski Sofia | 4.75 | 3.74 | 1.69 |
| 21:00 | 1612 | Cukaricki St vs Twente | 3.38 | 3.43 | 2.07 |
| 21:00 | 1708 | Sepsi Osk vs Djurgardens IF | 2.98 | 3.28 | 2.32 |
| 21:00 | 3178 | FC Vaduz vs Konyaspor | 6.06 | 4.24 | 1.49 |
| 21:00 | 5552 | FC Lugano vs Hapoel Beer Sheva | 1.92 | 3.54 | 3.74 |
| 21:15 | 4752 | Maribor vs HJK Helsinki | 2.23 | 3.22 | 3.22 |
| 21:30 | 1776 | Brondby vs FC Basel | 2.62 | 3.27 | 2.62 |
| 21:45 | 1075 | Vikingur Reykjavik vs Lech Poznan | 4.85 | 3.89 | 1.65 |
| 21:45 | 2565 | Linfield Belfast vs FC Zurich | 5.48 | 4.26 | 1.53 |
| 21:45 | 5186 | Breidablik vs Basaksehir | 5.85 | 4.13 | 1.52 |
| 21:55 | 5769 | Videoton FC vs Petrocub | 1.39 | 4.65 | 7.27 |
| 22:00 | 1663 | Al Masry Club vs Talaea El Gaish | 2.39 | 2.77 | 3.38 |
| 22:00 | 1977 | Olympiakos vs Slovan Bratislava | 1.38 | 4.64 | 7.66 |
| 22:00 | 2019 | Hajduk Split vs Vitoria Guimaraes | 2.37 | 3.33 | 2.88 |
| 22:00 | 3009 | Shamrock Rovers vs Shkupi Skopje | 2.21 | 3.29 | 3.18 |
| 22:00 | 5532 | Dundee Utd vs AZ Alkmaar | 4.97 | 3.80 | 1.65 |
| 22:10 | 2759 | Rosario Central vs Quilmes | 2.05 | 3.20 | 3.35 |
| 22:15 | 4532 | Throttur Vogum vs UMF Selfoss | 4.71 | 4.51 | 1.50 |
| 23:30 | 4754 | Atletico Huila vs Fortaleza (COL) | 2.96 | 3.15 | 2.25 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Agosti 4, 2022

Nipashe



## Pogba akataa kupasuliwa goti




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez wakionyesha mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 25 ambayo benki hiyo imetoa kudhamini maandalizi ya Tamasha la Simba Day litakalofanyika Agosti 8, mwaka huu jijini Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# SIMBA, YANGA DIMBANI OKTOBA 23

●●●Sasa mbio za kuwania ubingwa Bara rasmi zitaanza Agosti 15, mwaka huu kwa...

**Na Saada Akida**

MECHI ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi, Yanga na Simba imepangwa kufanyika Oktoba 23, mwaka huu kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mchezo huo utakuwa ni wa raundi ya nne katika msimu mpya wa 2022/2023 ambao utaanza rasmi ifikapo Agosti 15, mwaka huu, lakini ukitanguliwa na mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye uwanja huo huo.

Akizungumza jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo mechi ya marudiano kati ya vigogo hao wa soka nchini itapangiwa siku lakini itakuwa katika raundi ya 23.

Kasongo alisema pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara litafunguliwa rasmi Agosti 15, mwaka huu na litafungwa Mei 27, mwakani na siku hiyo michezo yote itachezwa kwa wakati mmoja.

Kasongo alisema msimu mpya utakuwa na michezo 240 na ratiba hiyo imezingatia mashindano mengine kama Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho Afrika na mashindano yote ambayo Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) itashiriki ikiwamo CHAN na AFCON.

"Katika ratiba tumezingatia pia kalenda ya FIFA kwa michezo ya kirafiki kwa timu za Taifa, mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Azam Sports Federation, lakini pia tumezingatia zoezi la kuhesabiwa la Sensa ambalo litafanyika Agosti 23, mwaka huu, hakutakuwa na mechi siku hiyo.

"Katika ratiba hiyo kutakuwa na mapumziko ya siku 17 kupisha masuala mbalimbali lakini pia mechi za Play Off kwa timu za Ligi Kuu zitachezwa Mei 31 na marudiano Juni 3, 2023," alisema Kasongo.

Alitaja mechi itakayochezwa Agosti 15, mwaka huu itakuwa ni kati ya Ihefu SC dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Highland States, Mbeya kuanzia saa 10:00 jioni wakati Namungo itawaalika Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi kuanzia saa 1:00 usiku.

Aliongeza mabingwa wa ligi hiyo, Yanga wataanzia ugenini Agosti 16, mwaka huu kwa kuwavaa Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha na siku itakayofuata Simba watawakaribisha Geita Gold FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 12: 15 jioni huku siku hiyo ni Azam FC ikiwaalika Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex kuanzia saa 2:15 usiku.

Mechi nyingine za raundi ya kwanza zitakuwa ni kati ya Singida Big Stars dhidi ya Tanzania Prisons (Liti, Singida), Mbeya City itawafuata Dodoma Jiji wakati Coastal Union itawaalika KMC FC kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

Katika kujiandaa na msimu mpya, timu zinaendelea na mazoezi huku zikiendelea na mchakato wa kusajili wachezaji wapya kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao.

Dirisha la usajili wa wachezaji litafungwa rasmi Agosti 31, mwaka huu na dirisha dogo litafunguliwa Desemba.

## CRDB yanogesha Simba Day, Okwa...

**Adamu Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI kiungo Mnigeria, Nelson Okwa akitarajiwa kutua nchini kesho, Simba imesaini mkataba na benki ya CRDB wenye thamani ya Sh. milioni 25 ili kunogesha Tamasha la Simba Day litakalofanyika Agosti 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema Simba Day ni siku muhimu kwa wapenzi wa klabu hiyo na siku yenye bashasha hata kwa wasio wachezaji ndio maana wameamua kufanya nao kazi.

"Tunatoa udhamini kwa tamasha hili ili liweze kufana, jambo la Simba ni jambo letu, ukizingatia michezo ni burudani na inajenga afya," alisema Nsekela.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez alisema anafuraha kuwatangaza CRDB kuwa wadhamini wa Simba Day msimu wa huu na kama klabu inawaheshimu nembo za wadhamini wote bila kujali rangi zao.

"CRDB ni wabunifu na tunafurahi kufanya nao kazi leo wametuonyesha uzito wa Simba day," alisema Barbara.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema katika kuelekea kilele cha Simba Day, viongozi na mashabiki wa timu hiyo jana walishiriki katika zoezi la kuchangia damu kwenye hospitali mbalimbali ikiwamo Hospitali ya Zakheim iliyopo Mbagala jijini.

Ahmed alisema wanaendelea na shughuli mbalimbali na kikosi chao kitarejea nyumbani leo mchana kikitokea Misri walipoweka kambi ambapo wachezaji watapewa mapumziko ya siku moja.

Alisema wamejipanga kurejesha mataji yote waliyopoteza msimu uliopita kwa sababu wamefanya usajili mzuri na baada kumtambulisha nyota mpya (Okwa), atabaki mchezaji mmoja ili kukamilisha usajili wao kwa wachezaji wa kigeni.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >